

EWE MWANA WA

DAUDI, UNIREHEMU



Hebu tuendeleo tu kusimama kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi. Ni wangapi wangetaka kukumbukwa usiku wa leo mbele za Mungu katika...?

² Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha sana kwamba Wewe huyajibu maombi. Shukrani sana kuona baada ya miaka mingi, kukutana na watu kutoka huko mbali katika miaka ya '46 na '47, wangali wameponywa, wakati walikuwa wakifa kwa kansa, viwete kwenye viti vya magurudumu, vipofu, wasingeweza kuona. Nao hawa hapa, hapa, wakinipa mikono, wakisema, “Ndugu Branham, nilikuwa kiwete; nilikuwa kipofu; nilikatiwa tamaa nikiwa na kansa, wala sijapata kuwa mgonjwa siku moja tangu wakati huo.” Ee Bwana, tunajua ya kwamba hiyo ingeweza tu kuwa ni neema Yako kwao. Tuna furaha sana kwa ajili ya jambo hili, nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba wengine ambao wanateseka leo hii watakumbuka ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

³ Tunaomba ya kwamba utatubariki usiku wa leo tunaposhiriki kwenye Neno lililoandikwa, kusudi utukufu wa Mungu upate kuingia miongoni mwetu. Tunashukuru sana kusikia matokeo ya mkutano wa usiku wa jana, kumpokea Roho Mtakatifu na kuokoka. Ee Bwana, jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya mambo haya. Tunaomba sasa ya kwamba utatubariki katika sehemu ijayo ya ibada tunapokungojea Wewe. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

⁴ Ni majaliwa makubwa sana kuwa na kusanyiko zuri kama hili kulizungumzia, na—na inalifanya rahisi sana kwako ku—kumwamini Mungu wakati haya, yanapotukia jinsi hii. Sasa, nimekuwa nikihubiri siku chache, na—na Injili tu, kwa kuwa ninafikiri kama—kama mtu ameponywa, kama wakiishi muda mrefu sana, wangali labda watakuwa wagonjwa tena. Lakini endapo wewe umeokoka, hiyo ni Milele, nawe unao Uzima wa Milele. Na ndivyo ilivyo... inachelewa sana katika nuru za jioni hata najisikia ya kwamba jambo moja kuu linahitajika zaidi ya yote: Hilo ni wokovu.

⁵ Nao uponyaji wa Kiungu ni ninii tu...Kama tu Ndugu Bosworth alivyoza kusema, “Uponyaji wa Kiungu ni chambo unachoweka kwenye ndoana. Samaki haoni ndoana; yeye humeza tu chambo akapata ndoana.” Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo. Watu huona ya—ya kimbinguni, maajabu ya mambo ya kimbinguni, Mungu akiwaponya wagonjwa. Ndipo wao—wao

wanayaendea hayo, na muda si muda mwajua, wao... muda si muda mwajua, wako moja kwa moja mikononi mwa Bwana Yesu pamoja na imani kuu ya kuamini. Ndipo—ndipo... kisha wanakuwa Mkristo, wana Uzima wa Milele.

⁶ Sasa, sehemu kubwa ya huduma ya Bwana wetu, yapata asilimia themanini yake ama zaidi, nafikiri ndivyo, inakadiriwa yapata asilimia themanini ya huduma Yake ilikuwa ni uponyaji wa Kiungu. Kwa hiyo Yeye alifanya hivyo kuyavutia macho ya umati, na pia kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi wao. Yeye aliwaonyesha ishara ya Masihi kusema ya kwamba walikuwa Masihi.

⁷ Jana usiku ninaamini Ndugu Arganbright aliliuliza kusanyiko kwamba ni wangapi wangetaka kuendelea ka—katika ibada za mahubiri, na ama ni wangapi wangetaka kwenda na kufanya ibada za uponyaji pekee. Nami nafikiri yapata, loo, asilimia ndogo sana kati yao walitaka ibada za uponyaji; lakini hata hivyo, kama tutaifungua mioyo yetu kwa Mungu, Mungu atafanya hivyo kwa vyovyote vile. Mnaona? Tunaliona tu jinsi hivyo.

⁸ Mchovu kidogo usiku wa leo. Nimekuwa... Nina popote kutoka ibada moja hadi tatu kwa siku, mwajua. Kwa hiyo ifikapo wakati ninapofika hapa karibu nimedhoofika sana tena kuanza. Kwa hiyo nilikuwa huko kwenye kanisa la kale la Pisgah alasiri ya leo, na ama Pisgah Home, vyovyote linavyoitwa; nami nawaambia, tulikuwa na wakati mzuri sana. Ninii... Nilikuta kwamba baadhi ya watu wa zamani waliotoka kwenye Mtaa wa Azusa wangali huko juu katika kanisa hilo, wakiabudu, ule Mtaa wa kale wa Azusa. Niliwaona hao wanawake wakongwe na wanaume wameketi pale. Ni—nilitaka tu kuwatupia mikono yangu na kuwakumbatia, mwajua. Wa—walionekana wa kupendeza sana.

⁹ Nafikiri mtoto m—mchanga sana, ama mzee, mwajua, wanaonekana kuwa wasiojiweza mara ya pili. Na mimi—mimi kweli, na—napenda kukutana na kijana na kujaribu kuwachochea kwenye njia ipasayo; kisha ninamwenda mzee na kutaka kujua ni mitaro mingapi aliyovuka na jinsi alivyoivuka, ndipo nitajua jinsi ya kuivuka ninapofika kule... Kwa hiyo—kwa hiyo, ninawapenda vijana na wazee, na walio katikati pia. Ninampenda kila mtu. Ni—ninaweza kusema hivyo kutoka moyoni mwangu.

¹⁰ Kama nilijua usiku wa leo ya kwamba nilikuwa na adui, huenda ikawa ninaye. Labda ninaye. Lakini endapo ninaye, sijui kabisa yeye ni nani. Kama nilikuwa naye, hakika nisingeanza kuhubiri mpaka niende, kwanza, na kuliweka hilo sawa, nione kama ningeweza kulinyosha, maana hatupaswi kuwa na lolote dhidi ya mtu yeyote, ama kukiweko na lolote tunaloweza kufanya, mtu yeyote na asiwe na chochote dhidi yetu. Mnaona?

Na sasa kama... Wala halisemi, “Endapo una neno dhidi ya ndugu,” bali, “kama ndugu ana neno dhidi yako,” unaona, “mwende,” unaona, “kama ana neno.” Na kwa njia hiyo, mbona, tunaishi kwa amani.

Ndugu Goad hapa, mvulana wa thamani... Wakati mwingine mtu fulani anasema, “Mbona... ufanisi wa ibada yako ni nini, Ndugu Branham?”

Hakika, ni Kristo.

“Unashikiliaje hivyo, na kuendelea tu usiku baada ya usiku?”

¹¹ Wavulana wangu, wa—watu walio pamoja nami; mvulana huyu hapa wakati mwingine huenda kwa siku kadhaa bila hata kula chakula, amelala kifudufudi, akimlilia Mungu apate kunisaidia. Sasa, Mungu kamwe hawezi kulikatilia tu hilo. Mnaona? Mke wangu nyumbani, watoto wangu, wapendwa wangu, watu, marafiki zangu, hufunga na kuomba. Huo hapo ufanisi.

¹² Mnaona, kila mmoja wetu... Sisi sote hatuwezi kuhubiri, na sisi sote... baadhi yetu hatuwezi kufanya jambo moja, lingine. Lakini sote tunaweza kufanya jambo fulani, na hilo husaidia. Mnaona?

¹³ Ni kama tu hii saa ya mkono hapa. Ina m—mkono, inaonyesha saa. Sasa, nisingejua ni mara ngapi kitu hicho kidogo kilienda huku na huku mle ndani kipate kuonyesha ni saa ngapi; mkono unaonyesha. Lakini kama gurudumu hilo dogo halikuwa likiruka huku na huku namna hiyo, ku—ku—ku—kusingekuwako na mkono wowote hapa kuonyesha wakati wowote. Mnaona? Nisingejua mahali ilipokuwa. Na kama kusingalikuwako na springi ya kuzungusha kutia majira kitu hicho kidogo kule juu, mbona, isingekuwika ikiruka huku na huku. Mnaona?

¹⁴ Kwa hiyo sisi—sisi... Kila kitu hakina budi kufanya kazi pamoja. Kanisa lote halina budi kuomba, na washirika wote hawana budi kuomba, mashemasi na wadhamini na mchungaji na sote pamoja tuje Mbele za Mungu namna hiyo, kama kitu kimoja kikuu.

¹⁵ Mnaona, sasa, tuseme kwa mfano, ile piano itatoa sauti. Ninajuaje? Ninajuaje kwamba itatoa sauti? Vema, ninaamini itatoa. Hivyo ndivyo ninavyoamini. Sasa, ungefanya nini kutoa sauti kwenye hiyo piano? Kidole changu kingepaswa kuigusa. Vema, sasa, jambo la kwanza, kichwa changu, akili yangu, haina budi kuliwazia. Moyo wangu hauna budi kuniambia kama itatoa ama la, hiyo ni kwa imani. Sasa, tuseme, kidole changu, ni kitu kikuu. Jicho langu, huo ni upande wa kinabii, kule kuona.

¹⁶ Vema, sasa, kama niliketi tu na kuiangalia hiyo piano, niseme, “Vema, itacheza,” vema hilo—hilo halinini—hilo

haliifanyi. Sasa, mnaona, sina budi kufanya... Miguu yangu haina budi kufanya kazi.

¹⁷ Sasa, vipi kama miguu yangu ikisema, “Vema, mimi si jicho, kwa hiyo kamwe sitafanya lolote kulihusu.” Vema, miguu ya—yangu iseme, “Nitakupeleka kule.” Vema, haya twende. Mnaona? Miguu yangu inanipeleka kule. Sasa, sasa, nipo hapa, nipo hapa. Vema, jicho langu lingali linaangalia, bali ha—ha—haliwezi kugusa kibao. Miguu inasema, “Vema, sigusi kibao.” Lakini inahitaji kidole. Mnaona?

Basi mnaona, kama—kama pua ikisema, “Nitakigusa,” hilo halitasaidia.

¹⁸ Jicho liseme, “Nitajaribu kukigusa,” halitasaidia. Mnaona? Itabidi kutumia kidole changu. Kwa hiyo kila kitu kikifanya kazi pamoja, [Ndugu Branham anacheza sauti fulani kwenye piano—Mh.] Nimefaulu. Mnaona? Jambo ndilo hilo.

¹⁹ Sasa, imani ni kitu gani? Kunazo hisi ngapi katika mwili wa binadamu? Tano: kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia. Hiyo ni kweli? Vema sasa, imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo usiyoyaona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia. Hiyo ni kweli? Ndiyo hisi ya sita. Kama ningalikuwa na juma lingine ningehubiri juu ya baadhi ya mambo hayo, hisi ya sita, ama, katika ibada ya uponyaji, hasa. Sasa, ni kama tu ninii yako...

²⁰ Njoo hapa, Ndugu Borders. Sasa, hebu niwaonyeshe. Hivi mmewahi kuwasikia watu wakisema, “Kuona ni kuamini”? Ni wangapi waliowahi kusikia hilo? Loo, mmelisikia, “Mimi ni Missouri,” mwajua, “huna budi kunionyesha.”

²¹ Na sasa, yupo mtu aliyesimama mbele zangu. Ana nywele za hudhurungi, amevaa suti inayoonekana kidogo kama ya hudhurungi, tai ya hudhurungi pamoja na shati jeupe. Ni wangapi wanaamini hilo? Mnaona? Vema, sasa nina hisi moja ambayo inatangaza kwamba yupo hapo, hiyo ni macho yangu. Sasa, rudi nyuma kidogo tu. Vema, sasa, haiwezekani kwangu, hisi yangu ya kuona iseme yupo hapa, bali ninajua yupo hapa sasa kadiri tu ninavyojua ninamwangalia. Kwa nini? Siwezi kumwona. Mnataka kubishana nami yeye hayupo hapo?

Sasa, mnasema, “Labda ulimsimamisha Ndugu Buntane.” Loo, la, la, la, la. Si Ndugu Buntane, ni Ndugu Roy—Ndugu Roy Borders.

²² “Unajuaje ndivyo ilivyo? Umeushika tu mkono wa mtu.” Hamjanibadilishia watu. Yeye amevaa pete pana sana ya arusi, mnaona, nami ninajua huyo ni yeye. Mnaona? Kwa hiyo ni—ninajua huyo ni... Sasa, siwezi kumwona, bali ninajua yeye yupo hapo vizuri tu kama kwamba nilikuwa nikimwangalia. Kwa hiyo kuona si kuamini, sivyo? La, la, huh-uh, sio wakati huu. Hakika sivyo, kwa maana kugusa ni kuamini. Hiyo ni kweli?

²³ Vema, sasa. Angalieni sasa, ni kitu gani... (Asante.) Imani ni nini? Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya moja kwa moja ya mambo usiyoyaona, kuonja, kugusa, kunusa, wala kusikia. Mnaona? Jambo ndilo hilo. Unasema, “Shati lile ni jeupe.”

Vema, vipi kama ningekwambia, “Shati lile ni jekundu.”

Ungesema, “Ngoja kidogo, Ndugu Branham, shati lile ni jeupe.”

²⁴ Vema, ningesema, “La, ni jekundu.” Vema, sasa, jinsi tu lingaliweza kuwa... Ingewezekana lingeweza kuwa ni jekundu? Naam. Kama ulikuwa na upofu wa rangi huenda likawa jekundu. Unaona? Kwa hiyo kuona kusingekuwa ni kuamini bado. Unaona?

²⁵ Lakini imani yako... Wakati imani ni hakika, unaweza kuwa sio... kuwa na hakika sana. Kama vile ikiwa umeketi kwenye—kwenye—unafanyiwa ke—kesi, kwenye kesi nawe uliangalia dirishani na kuona ajali. Ni vigumu kwao kuchukua ushahidi wako, maana huenda uliona mazingaombwe. Kamwe hukuiona hivyo. Unaona? Na wakati mwingine unafikiri una hakika kabisa.

²⁶ Uliwahi kushuka barabarani na kuona mazigazi barabarani? Yanafanana na maji kabisa. Nilisoma gazetini hapa wakati fulani uliopita ambapo kundi la bata walidhani yalikuwa—yalikuwa ni maji, na hapana shaka waliyaona pale kwa macho yao, nao wakashuka moja kwa moja barabarani. Iliwaua wote, mnaona, kwa kuwa ilikuwa ni mazigazi.

²⁷ Mara nyingi wanadamu huona mazigazi, nao wanafikiri, “Loo, hili ndilo hasa,” wanaishia kujiua. Mnaona? Waangalieni huko nje jangwani wanapokuwa huko nje wakitafuta madini. Wanaishiwa na maji, na kantini yao imeishiwa, wala hawana maji. Ndipo wao—wanaanza kuona mazigazi nao wanadhani ni maji, nao wanakimbia na kuanguka na kuanza kujitupia, wanafikiri, maji juu yao. Basi ni kitu gani? Wanajifunika kwa mchanga wenye joto. Na hivyo ndivyo ibilisi hufanya. Wakati mwingine anakuonyesha mazigazi ya uongo. Nawe unafikiri ni kitu fulani kikuu, bali unapofika kule, unajikuta ukijifunika tu kwa mchanga wa moto na dhambi juu yako zaidi na zaidi. Unaona, usifuate mazigazi ya ibilisi; acha imani yako itie nanga moja kwa moja katika Neno la Mungu. Dumu moja kwa moja nalo, unaona, namna hiyo. Halina budi kukuvuta utoke. Unaona?

²⁸ Hiyo hisi ya sita ita—ita—itaenda kinyume na yoyote ya hizo zingine tano. Tunafanya... Hizo tano ni sawa maadamu zinakubaliana na ya sita. Bali mwanadamu hakupewa kuishi kwa hizo hisi tano; alikuwa... kuachilia hizo hisi tano zimwongoze. Alipewa, anaelekea, alizaliwa hapa apate kuongozwa na hisi ya sita, hiyo ndiyo sababu ya Mungu

kumpa hisi ya sita. Hapo ndipo mahali pa Mungu moyoni pa kutuongozea. Kwa hiyo tunaongozwa na hisi ya sita, ikiwa tu tutairuhusu. Sasa, kama hisi ya sita ikisema ya kwamba Ne—Neno limekosea, basi usininii, wewe huko kwenye hisi ya sita. Unaona? Hizo ni zile hisi tano, lakini hisi ya sita itaamini mambo ambayo zile hisi tano haziyatangazi. Kidogo linatataniisha bali ni—ni kweli, mnaona, ya kwamba hisi ya sita ndiyo inayotuongoza.

²⁹ Mimi, huko nje dakika chache zilizopita, ndio kwanza nimwombee mwanamke mpendwa mkongwe ambaye amelala pale kwa muda wa siku nne akingojea kuombewa. Na kitu kama hicho, nawaambia, ninajisikia tu kana kwamba ninapaswa kuibadilisha iwe ibada ya uponyaji kwa namna fulani, kumwona Roho wa Mungu akitenda kazi namna hiyo. Maskini kizee huyo, nilimshika kwa mkono, na—nami nikaona shida yake. Na vema, hiyo. . .

³⁰ (Mlisoma nini sasa? Luka, naam, uh-huh, vema.) Sasa, ninataka kuchukua somo kutoka hapo, Bwana akipenda. Sasa, Mungu akipenda, kesho usiku niliahidi, ninataka kuhubiri juu ya *Muhuri Wa Mungu*. Nyote mnapenda masomo ya kufundisha kama hayo? *Muhuri Wa Mungu*, halafu basi *Alama Ya Mnyama* kesho yake usiku. Basi usiku wa leo ninataka kuchukua somo kutoka kwa hili, ama, kwa ajili ya somo, kutoka mahali ambapo amesoma hapa, Luka Mtakatifu m—mlango wa 18. Naye alisoma kutoka kwenye kifungu cha 35 hadi 43, vyote pamoja.

³¹ Sasa, ninataka kuchukua kifungu cha 38 kwa ajili ya somo. *Ewe Mwana Wa Daudi, Unirehemu*. Basi hebu tulichukue zaidi kama mchezo wa kuigiza usiku wa leo. Nimechoka kidogo kooni mwangu, na hebu na tufanye tu mchezo mdogo wa kuigiza kwa dakika chache.

³² Onyesho le—letu linaanza kwenye asubuhi baridi, ya majira ya kuchipua, na iko kwenye zile kuta, zile kuta za kale zilizobomolewa za Yeriko. Na kuna m—mtu ameketi pale ambaye tunajua kuwa ni ombaomba jina lake Bartimayo kipofu, ama Bartimayo; lingekuwa ni mojawapo, likitamkwa vizuri. Na kwa hiyo katika siku hiyo kulikuwako na ombaomba wengi. Na usiku kucha alikuwa amegaagaa na kubingirika, asingeweza kulala. Wengi wetu tunajua vile usiku wa aina hiyo ulivyo, hakuna raha hata kidogo. Naye angebingirika kutoka upande mmoja wa kitanda hadi mwingine, wala hapakuwapo na raha kwa maskini jamaa huyo mkongwe. Naye alikuwa ameamka amechelewa, kwa hiyo alikuwa amekuja kituoni pake amechelewa. Kwa hiyo, kama—kama hawako huko mapema, wafanyabiashara na kadhalika, wakiingia, kuna ombaomba wengi sana pamoja na watu, wasiotibika, kama vile upofu, na ukoma, na viwete, na kadhalika, na watu waliokuwa ni maskini. Na yapata ombaomba wa kwanza waliyekutana naye walimpa sarafu, na hiyo karibu ilitosha. Hiyo tu ndiyo wangaliweza kutoa siku hiyo.

³³ Kwa hiyo alikuwa amekuja kituoni pake amechelewa. Hebu tuseme ni karibu saa mbili asubuhi, naye alipaswa kuwa pale yapata thenashara. Lakini sababu ya kuchelewa ni kwamba alikosa usingizi mwingi mno. Usiku kucha alikuwa amebingirika na kugaagaa wala asingeweza kulala. Naye angeninii... alikuwa akiota usiku kucha ya kwamba angeweza kuona tena. Aliota kwamba aliweza kuona. Naye angeamka, angerudi kulala.

³⁴ Mnajua ninaamini Mungu hutuonya mara nyingi katika ndoto. Hamwamini hivyo? Sikuzote ametuonya, na Yeye aliahidi katika siku za mwisho ya kwamba angeonyesha maono na kuwajalia waote ndoto. Basi hebu tumwazie Bartimayo, naye aliota ya kwamba angeweza kupu... alikuwa amepata kuona kwake na angeweza kuona tena.

³⁵ Kwa hiyo wakati alipofika pale asubuhi hiyo alikuwa amechelewa, na wafanyabiashara wote walikuwa tayari wameingia mjini, na—nao huo mji mkuu wa biashara, kama ulivyokuwa. Lakini wote—wote walikuwa wameingia, wakafika mapema sokoni kuuza bidhaa zao na kadhalika. Kwa hiyo labda ingembidi abaki bila siku hiyo. Hakuwa... hatapata sarafu yake ya siku hiyo ya kulia. Nami ninaweza tu kuwazia, kama vile mara nyingi tumemwazia: amevaa joho lake la kale, lililochakaa, namna *hiyo*, na maskini mikono yake iliyokonda, na ndevu kote usoni mwake, na hizo za kijivu, na—na kipofu barabarani, kidogo akijaribu kufika mahali ambapo angeketi chini na kuomba. Kila mmoja alikuwa na mahali pao pa binafsi ambapo wangeomba.

³⁶ Hilo ni jambo la kuhuzunisha. Nimekuwa India na kuwaangalia huko ambako kuna—kuna watu milioni mia nne na sabini katika India; na kusema kweli, karibu ningesema milioni mia nne wao ni ombaomba. Ninyi... Kila mahali tu ni ombaomba, ombaomba, ombaomba. Na kila mmoja wao anayo nguzo na mahali pao, na namna fulani ya mazingaombwe wanayofanya kuuvutia usikivu wa watalii: na ni mandhari ya kusikitisha sana.

³⁷ Halafu tunamwona ameketi pale. Na baada ya usiku mbaya, vema, aliona hapakuwapo na mtu pale, kwa hiyo akawazia labda angeketi chini juu ya jiwe. Mnajua zile kuta zilikuwa zimebomolewa katika siku zake kutoka pale Yoshua alipoingilia, na mawe makubwa yalikuwa yamewekwa huko nje upande mmoja. Kwa hiyo hapana shaka alipata njia ya kutokea upande mmoja wa lango la kaskazini linaloelekea Yerusalemu. Ndipo akaketi chini pale kwenye jua. Naye alikuwa akiwazia, “Vema, majira ya kuchanua yanakuja sasa, nami ninaamini nitaketi tu hapa kwenye joto la jua; Ninasikia baridi asubuhi ya leo, na nguo zangu ni nyepesi. Nitaketi tu hapa kwenye joto la jua kwa muda kidogo, na—na huenda kuna mmoja aliyesalia ambapo

ningeweza kupata sarafu yangu. Nisipopata, familia yangu ita—itaona njaa leo.”

³⁸ Basi wakati akiketi pale alianza kuwazia juu ya ndoto yake: “Jana usiku niliota ya kwamba ningeweza kuona. Loo, jinsi ambavyo hapana shaka anga zinaonekana nzuri. Milima inaanza kuchanua tena.”

³⁹ Ndipo mawazo yake yanarudi kwenye wakati alipokuwa mvulana mdogo wakati alipokuwa akiishi karibu na ufuko wa Yordani, na mapema kwenye majira hayo ya kuchipua, mbona, vikombe-mtindi ingechipusha, na hayo maua madogo. Jinsi, mvulana mdogo, jinsi alivyokuwa akitembea—tembea mlimani na kuketi chini na—na kuchuma hayo maua, na kukaa huko, na loo, asubuhi, na kuwazia jinsi ambavyo anga zilikuwa zinapendeza, na hayo mawingu makubwa meupe yakiingia kwenye majira ya kuchipua, na—na jinsi ambavyo mimea ilikuwa ikichipusha, jinsi anga zilivyokuwa bluu, nayo Yordani katika majira yake ya kufurika, theluji ikishuka kutoka Yuda, na jinsi ambavyo maua yalikuwa yakichanua.

⁴⁰ Ndipo basi angesikia sauti inayojulikana ambayo sote tunapenda kuisikia, sauti tamu ya mama, ikiita, “Bartimayo, mtoto wangu mdogo, chakula chako cha mchana kiko tayari.” Na halafu wakati baba yake alipokuwa kondeni mahali fulani akifanya kazi, jinsi ambavyo angeingia, jinsi ambavyo maskini mama huyu wa Kiyahudi angemngojea kwenye vipandio, na kumchukua mikononi mwake, na kumkumbatia, na kumketisha chini kwenye cha—chakula chake cha kutwa.

⁴¹ Halafu basi baada ya kumaliza, alienda barazani. Naye alikuwa akiketi nje barazani, na jinsi mama yake angempembeza, ndipo ingembidi kulala kidogo alasiri. Kwa hiyo angezichanua nywele nyuma kutoka machoni mwake, na—naye... angeangalia juu na kuona hayo macho mazuri, makubwa, mororo ya mama, na jinsi angeyabusu mashavu yake madogo na kusema, “Loo, jinsi ninavyomshukuru Yehova Mungu mkuu kwa ajili ya maskini mvulana mdogo mzuri kama wewe, Bartimayo. Unajua, Bartimayo, ulipozaliwa nilikuweka wakfu kwa Yehova. Sikuzote nimeamini ya kwamba Yehova atakutumia wewe siku moja, Bartimayo, Yeye atakutumia kwa utukufu Wake.”

⁴² Kisha angewazia, “Mimi huyu hapa nimeketi hapa kipofu, labda si zaidi ya maili moja kutoka mahali nilipochezea na nikapaona. Basi Yehova angeweza kunitumia mimi? Mimi ni kipofu. Hakuna matumaini kwangu.”

⁴³ Lakini sikuzote hatujui, mwajua. Mungu hufanya kazi katika njia za ajabu kutenda maajabu Yake. Kama tukikabidhi chochote kwa Mungu na kuamini, kama vile watoto wetu na chochote kile, hebu tuamini ya kwamba Mungu atayajibu maombi hayo. Leo hii kabla sijaondoka kwenda, huku simu

ikilia kila mara, nao mama pamoja na watoto wao na kusema, “Sasa, waombe.”

⁴⁴ Ninasema, “Sasa, wakabidhi tu kwa Mungu. Hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya. Wala usiweke mikono yako juu yake tena. Acha Mungu amchukue. Kama utafanya jambo fulani juu yake, basi Mungu atasimama kando na kukuacha uendelee mpaka utakapomaliza. Lakini wakati unapolikabidhi kwa Mungu na kumwacha awe nalo, basi Yeye atafanya hivyo.” Wewe—wewe mwamini tu. Simama tu kando, na usifanye kazi, bali amini. Hapo ndipo neema inapohesabiwa kuwa haki, kuamini kwamba Mungu atatenda.

⁴⁵ Ndipo akasema, hapana shaka, moyoni mwake, kwamba alikumbuka jinsi ambavyo mama alikuwa akimsomea hadithi za Biblia. Mnajua ilikuwa akina mama walikuwa na wakati wa kuwasomea watoto wao hadithi za Biblia; hawanao tena sasa. Inawabidi kununua gari jipya na kutoka nje na kwenda kwenye karamu za wanawake za karata, na—na kila kitu.

⁴⁶ Nao mama, ilikuwa kwamba, iliwabidi kubeba maji yao kutoka kwenye chemchemi na kuyachemshia nje. Ninakumbuka mama yangu ana birika kubwa mno la chuma la kale, naye anafulia nje naye alikuwa na wakati mwingi zaidi, sasa, kuliko mama wa kisasa alio nao kubonyeza tu kitufe, namna *hiyo*, na kufua, vyombo, na kadhalika, kubonyeza tu kitufe. Lakini sidhana manufaa yetu ya kisasa yametufikisha mahali popote. Na jambo ni kwamba, yametufanya wazembe sana, yakituaa kwa ugonjwa wa moyo na kila kitu kingine.

⁴⁷ Susanne Wesley alikuwa na watoto kumi na saba. Na pamoja na hao watoto kumi na saba huko nyuma mamia ya miaka iliyopita, angali angeweza kuchukua kutoka saa mbili hadi tatu kwa siku, katika ratiba yake yote yenye shughuli nyingi, kusoma Injili na kuwaombea watoto wake. Kulifanyika nini? Alikuwa na John na Charles, kutoka huko ndani, ambao waliupindua ulimwengu juu chini. Susanne Wesley, nilisimama karibu na kaburi lake sio muda mrefu uliopita na kuweka mkono wangu kwenye lile jiwe. Nikasema, “Mungu, ipe Marekani mama wengine kama huyo.” Hiyo ni kweli. Alitoa Charles na—na John Wesley.

⁴⁸ Charles aliupa ulimwengu baadhi ya nyimbo nzuri sana za Injili. Naye John, loo jamani, alikuwa—alikuwa ni kijinga cha moto kilichonyakuliwa kutoka motoni. Hiyo ni kweli. Jinsi yeye alivyokuwa ni mtu mkuu wa Mungu.

⁴⁹ Sasa, lakini siku hizi pamoja na manufaa yetu yote ya kisasa, na badala ya kuwasomea watoto wetu Biblia, tutaifungua televisheni na kuwaacha waangalie kitu ambacho hata hakifai kwao kuangalia. Sasa, hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Na jambo lingine, tutawapa maskini vitabu hivi vya katuni, na maskini vitabu vya hadithi kutoka kwenye . . . rafu za baadhi ya duka za

dawa za kulevywa ambazo hata hazifai kuuzwa ku—kutengeneza vijiti vya kuwashia moto, ama kuwashia moto. Na hata hivyo tunashindilia upuuzi wa aina hiyo yote shingoni mwa watoto wetu. Mbona, Wamarekani. . .

⁵⁰ Ninabashiri wapo, kwamba karibu kila mvulana Marekani anaweza kukwambia Davy Crockett alikuwa ni nani. Lakini nadhani hakuna theluthi moja yao wanaoweza kukwambia Yesu Kristo alikuwa ni nani. Hiyo ni kweli. Loo, Komando Mpweke, ama mtu kama huyo, ama mcheza sinema fulani, wanajua yote kumhusu kwa sababu imewekwa mbele zao.

⁵¹ Nayo Biblia ni Kitabu kinachowekwa kando ndipo wakati mhudumu anapokuja, wanakichimbua, na kukipangusa vumbi na kukiweka juu *hivyo*. Kamwe haisomwi. Tunachohitaji siku hizi ni akina mama wazuri wa mtindo wa kale warudi wakawarudishe watoto wao kwenye maombi. Hiyo ndiyo tiba iliyo bora sana niijuayo ya kutibu uhalifu wa watoto, hiyo ni kweli, ni maskini akina mama waaminifu.

⁵² Ninawasikia wakizungumza juu ya ukosefu wa elimu wa akina mama wa Kentucky huku karibu katika sehemu hii ya nchi tunakotoka, huko juu. Sasa, labda wao, wasingeninii. . . huenda wasijue mkono wa kuume na wa kushoto lakini acha mmoja wa wasichana wao aingie usiku mmoja huku nywele zao zimepinduliwa, na nguo zake zote zimetoka, na rangi ya midomo imepakwa kote usoni mwake na jinsi hiyo, na maskini mhuni aliyelewa nusu, wa manjano, anayevuta sigara amlete binti yake kwenye mapambazuko: Nakwambia, hataweza kutoka kitandani kwa muda wa miezi mitatu. Nitawahakikishia tu jambo hilo sasa. Naam, bwana. Mnanena juu ya kutokuwa na elimu, sisi. . .hiyo ni. . .Tunahitaji mama wengine wa aina hiyo (Naam, bwana, naam, bwana.) watakao—watakaoirejesha nidhamu.

⁵³ Nyumbani mwetu tulikuwa na Amri Kumi, zilitundikwa juu ya mlango, hikiro yenye hizo zote kumi, huko mwishoni namna *hiyo*. Nami nawaambia, tulipata—tulipata elimu yetu kutokana na hizo. Um-hum. Hiyo ni kweli. Ninaweza kumwona baba yangu, bado, akiunyosha mkono na kusema, “William. . .”

Ningesema, “Loo, jamani.” Nilijua kilichokuwa kinafuata. Ila na—nashukuru kwamba alifanya hivyo. Hiyo ni kweli.

⁵⁴ Bartimayo angewazia juu ya maskini mama yake wa thamani, jinsi alivyozoea kumwambia hadithi za Biblia kuhusu yale Bwana aliyofanya. Angesema, “Bartimayo, unajua, sisi Wayahudi, kwa uchaguzi wa Mungu, Yeye alituchagua kuwa watu Wake kwa sababu tulimpenda na kumtumikia. Bartimayo, huenda ukaishi kuwa mtu mashuhuri siku moja. Ninakutarajia kuwa mfalme wa Israeli. Ni—ninakutaka uwe. . .” Matarajio ya kila mama ni mtoto wake awe kitu fulani kikuu, na hivyo ndivyo anavyopaswa kuwa. Naye akasema, “Nimeomba. Nami. . .

nilipojua ulikuwa unakuja duniani, wakati Mungu alipokuweka chini ya moyo wangu, vema, ni—niliyakabidhi maskini maisha yako kwa Mungu. Nawe unajua ninataka umtumikie Mungu huyu mkuu. Nitakwambia jinsi Yeye alivyo mkuu, Bartimayo. Nawe unajua tulikuwa tukitoka Misri. Tulikuwa watumwa wakati mmoja, Naye akatutoa huko Misri, jinsi ambavyo aliifungua Bahari ya Shamu, akawalisha wana wa Israeli kutoka Mbinguni kwa mana, akawapulizia nyama, kware kwa ajili yao, akawapa maji kutoka Mwambani katika jangwa, na yale mambo yote makuu aliyofanya.”

Na, loo, maskini macho yake maangavu yangeninii tu . . . Angesema, “Loo, mama, huyo Yehova mkuu, angali hai bado?”

“Loo, naam, kipenzi. Yeye ni yule yule tu kama alivyowahi kuwa. Angali ni Yehova.”

⁵⁵ Alikuwa akiipenda hadithi hiyo, na kusimulia jinsi ambavyo wa—wana wa Israeli walikuwa . . . kasema, “Moja kwa moja kule chini kwenye kile kivuko cha maji mafupi, siku moja yule Yoshua mkuu, mwenye nguvu alivuka moja kwa moja pale pamoja na wana wa Israeli. Karibu tu na ule mji ambako tunaenda kununua vyakula vyetu huko chini Yeriko, Yoshua alivukia pale pale, yule shujaa mkuu, mwenye nguvu, mtumishi wa Mungu. Jinsi ambavyo Musa alisimama huko juu ya mlima, akaangalia huko kwenye mawimbi yaliyofurika ya huo mto, na jinsi ambavyo asiyeamini alidhanja, ‘Huu ni wakati mzuri. Tuko salama. Mungu ni mhandisi hafifu, kuchagua wakati huu wa mwaka kuvukia.’ Lakini Mungu wakati mwingine huchukua tu saa iliyo mbaya kuliko zote kuthibitisha kwamba Yeye ni Mungu.” Naam, bwana. Inaonekana kana kwamba angewachukua wakati mto . . . awalete huko juu wakati maji yalikuwa chini. La, hilo silo. Yeye anataka tu kukuthibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu. Yeye—Yeye anapenda kudhihirisha utukufu Wake.

Na loo, ninapenda tu hilo. Ninapenda tu hilo, kuona na kujua ya kwamba Yeye ni Mungu.

⁵⁶ Kisha moja ya hadithi ambazo Bartimayo alipenda vizuri sana ilikuwa ni ile hadithi ya mwanamke Mshunami, kwa kuwa ilikuwa na mvulana mdogo ndani yake, mwajua. Kuna mvulana mdogo mle ndani ambaye . . . Naye angesimulia habari za nabii yule mashuhuri mwenye nguvu, Elisha, jinsi ambavyo Mungu alimfanya kuwa nabii mkuu sana, mwenye nguvu. Aliishi nyikani wala hakuwa na nguo nyingi, naye alijizungushia kipande cha ngozi, na—na jinsi alivyokuwa ni mtu mashuhuri mwenye nguvu wa Mungu, hata hivyo. Aliishi chini ya upako wa Mungu. Naye angepitia kwenye mji fulani, na kulikuwako na mwanamke Mshunami pale. Naye alikuwa ni mwanamke mkarimu, na alimpenda Mungu pia. Ingawa ni Mmataifa, a—alimpenda Mungu.

57 Nami huenda nikasema ya kwamba huenda alimwambia Bartimayo, “Unajua, Bartimayo, sisi ni watu waliochaguliwa na Mungu lakini siku moja atakuja Masihi mkuu. Basi wakati Yeye ata . . . atakapokuja, atakuwa Ndiye atakayewaita mataifa wote, kwa kuwa mwanamke huyu Mshunami. . . Mungu anawapenda wote watakaopendeka. Yeye anataka kuja na kuwasaidia wale wanaotaka kusaidiwa.

58 “Pia Bartimayo, mwanamke huyu mashuhuri, angemwona mtu huyu mtakatifu akipitia mjini. Kwa hiyo alitaka kumpa fadhili, kwa sababu alimpenda Mungu, naye alijua huyu alikuwa ni mtumishi Wake, naye alitaka kumsaidia na kumfanyia jambo fulani. Kwa hiyo ange—angemwona akija, naye angetoka na kumwomba aingie na—na kukaa pamoja nao. Kwa hiyo mumewe kwa namna fulani alikuwa ni tajiri. Kwa hiyo siku moja akamwambia mumewe, ‘Unajua, mpenzi, mtu huyu mtakatifu mashuhuri wa Mungu hupitia hapa, naye anapanda kule juu kwenye pango ambamo anaishi, huko juu ya Mlima Karmeli. Kwa hiyo wakati akipitia hapa, ninaamini lingekuwa ni jambo zuri kama tungemjengea chumba kidogo tu kando ya nyumba yetu. Ninaamini hilo lingekuwa ni jambo zuri sana kama tungefanya hivyo, kwa sababu sote wawili tunamwamini Mungu, Naye ni Mungu, na huyo ni mwakilishi wa Mungu. Huo ndio wito wa juu sana duniani sasa wa Mungu ni mwakilishi Wake.

“Kwa hiyo mumewe akasema, ‘Nafikiri hilo litakuwa sawa.’ Kwa hiyo wakajenga nyumba ndogo huko.

59 “Basi siku moja wakati Elisha na Gehazi, m—mtumishi wake, walipopitia hapo nao wakaona chumba hiki kidogo kimejengwa pale na wakaingia. Walikuwa na kitanda kidogo kizuri mle, na—na kiti kidogo na maji na kila kitu. Kwa hiyo kasema, ‘Nenda ukamwulize Mshunami huyu nimfanyie nini. Amekuwa mwema sana kwetu; labda tungeweza kumrudishia fa—fadhili. Labda angetaka nizungumze na mfalme, ama labda angetaka nizungumze na jemadari mkuu ama mtu fulani.’

60 “Lakini unajua, Bartimayo, kile mwanamke huyo, yeye hakuomba kitu chochote. Lakini Gehazi aliporudi, alisema, ‘Nakwambia, Elisha, nabii mkuu wa Mungu, mwanamke huyo ni tasa. Hana watoto. Kamwe hajapata kuwa na watoto wowote.’”

61 Ndipo kasema, “Bartimayo, unajua mama yeyote anataka mvulana mdogo mzuri, kama ulivyo wewe. Unaona? Hiyo ndiyo sababu Yehova ni mwema sana kwangu kunipa wewe. . . kunipa mvulana mdogo kama wewe. Naye maskini mama huyo alitaka mvulana mdogo kama wewe.

62 “Kwa hiyo Elisha akasema, ‘Nenda, mwambie aje asimame mbele zangu.’ Na kwa hiyo, hapana shaka ila Elisha aliona ono la jambo la kufanya. Kwa hiyo basi wakati mwanamke huyo alipoingia, yeye alisema, ‘Kulingana na majira ya uhai, utamzaa mwana.’ Ndipo akatoka. Nawe wajua nini, Bartimayo? Huyo

mama alimpokea mvulana mdogo mzuri, mvulana mdogo tu wa Kimataifa, kama tu vile wewe ulivyo mvulana wa Kiyahudi. Jinsi mama huyo alivyompenda mvulana huyo mdogo. Jinsi hapana shaka aliwazia yeye alikuwa kitu kilicho kizuri kuliko vyote.

⁶³ “Ndipo wakati alipokuwa na umri wa yapata miaka kumi na mmoja, siku moja aliambatana na baba yake huko shambani ku—kuvuna. Nami ninaamini hapana shaka alipatwa na jua kwa kuwa alianza kusema, ‘Kichwa changu, kichwa changu.’ Akazidi kuwa mgonjwa zaidi na zaidi.

⁶⁴ “Kwa hiyo baba akiwa na shughuli nyingi sana pamoja na wafanyakazi, alimwagiza mtumishi kumwingiza ndani maskini jamaa huyo, na kumweka kwenye paja la mama yake. Alimweka pajani mpaka yapata aduhuri, ndipo pumzi yote ikamwishia na maskini mvulana huyo akafa. Sasa, lakini Bartimayo, ninataka uone yale maskini mwanamke huyu Mmataifa, sasa, yale aliyofanya. Alimwingiza ndani na kumlaza juu ya kitanda cha nabii.”

⁶⁵ Sasa, huo hapo ufunuo wa ajabu. Mnaona? Hakumpeleka kwenye kitanda chake mwenyewe; wala hakumweka kwenye kitanda chake, ama kitanda cha babaye. Yeye alimchukua akamlaza kwenye kitanda cha nabii kwenye chumba ambamo nabii alikuwa amelala.

⁶⁶ “Kisha akamwambia mumewe, ‘Tandika nyumbu; nawe nitangulie sasa,’ akamwambia mtumishi, ‘wala usisimame. Mtu yeyote akikusalimia, usimjibu, bali nenda moja kwa moja kwa huyo mtu wa Mungu juu ya Mlima Karmeli.’

“‘Sasa,’ kasema, ‘Sasa,’ mumewe akasema, ‘sio mwandamo wa mwezi, wala si Sabato, kwa hiyo mtu wa Mungu hatakuwa kule.’

“Akasema, ‘Yote yatakuwa ni sawa.’”

Ninapenda hilo, wakati unapokuwa na huo mshiko halisi wa imani, um-hum, dumu kwenye hiyo. Hilo ni somo zuri kwenu nyote akina Bartimayo sasa. Angalieni.

⁶⁷ “Kisha akasema, ‘Nenda! Twendelee mbele, usisimame kwa wito wa kijamii na kadhalika. Twendelee tu mbele; endelea tu kusonga. Usisimame mpaka nitakapokwambia usimame.’ Na bila shaka, alipokaribia Mlima Karmeli, wakati nabii . . .”

Mwajua, Mungu hawafunulii manabii Wake kila kitu. Sote tunajua hilo. Yeye huwafunulia tu manabii Wake kile anachowataka wajue.

⁶⁸ “Na sasa wakati alipofika karibu, Elisha alijitokeza, labda ni mzee na labda macho hayaoni vizuri. Akainua mikono yake juu na kusema, ‘Huyu hapa Mshunami yule anakuja, naye anaonekana kana kwamba ana fadhaa. Lakini Mungu amelificha kwangu.’ Kwa hiyo akamwambia Gehazi, ‘Toka uende

ukamwite.’ Lakini alikuwa akienda kasi sana. Wakati alipofika pale alipaza sauti, ‘Hujambo? Mumeo hajambo? Mtoto wako hajambo?’

“Basi angalia yale mwanamke huyo aliyosema. ‘Hatujambo.’”

Amina. Mnaona, yeye alijua kwamba Mungu alikuwa ndani ya nabii huyo. Hiyo ni kweli. Alijua ya kwamba huo ulikuwa ndio wito wa juu sana alikuwa nao Mungu siku hizo.

⁶⁹ Nafikiri hapo ndipo Martha alipopata lile wazo; hapana shaka aliisoma hadithi hiyo. Wakati Lazaro ndugu yake alipofariki, yeye alijua kama Mungu alikuwa katika nabii huyo, Mungu hakika alikuwa ndani ya Mwana Wake. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo akamwendea na kusema, “Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Ninapenda hilo. Ninapenda hilo. Mnaona, hilo lilimshtusha. Mnaona, “Hata sasa lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.”

⁷⁰ Maskini mvulana huyu anayeketi hapa amepondwa mguu, jamaa mwingine mdogo anayeketi hapa; niliwaona wote wawili wakipaza sauti jana usiku. Hapana shaka ni wavulana Wapentekoste, hapana shaka wanaye Mungu moyoni mwao. Unasema, “Ndugu Branham, labda sitatembea tena. Daktari anasema sitatembea.” Huyu hapa mwenye ugonjwa wa moyo, huyu aliye na *chochote kile*; hata shida yako iwe ni nini, sema, “Vema, daktari anasema sitapona. Kamwe sitaweza kupona huu. Nina kansa. Nina uvimbe. Nina *hiki-na-hiki*.”

⁷¹ “Lakini hata sasa, Bwana, lolote utakalomwomba Baba, Yeye atakupa.” Jambo ndilo hilo. “Hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Hapana shaka hapo ndipo Martha alipopata hadithi hiyo.

⁷² “Huyo mwanamke Mshunami alisema, ‘Hatujambo.’ Sasa, hakuwa akiomba kwa ajili ya huyo mvulana, bali yeye alijua ya kwamba Mungu aliweza kupitia kwa nabii huyu kumwambia ni kwa nini alimchukua mvulana huyo na hilo lingemridhisha. Kama angeweza kusema ni kwa nini Yeye alimchukua huyo mvulana, kila kitu kilikuwa ni shwari. Kwa hiyo alikuwa mbele ya mwakilishi wa Mungu, na mambo yote yalikuwa ni shwari.”

⁷³ Ninawazia macho ya maskini Bartimayo yangeangaza tu. “Mama, mama, harakisha. Niambie yaliyotukia.” Mnaona, wavulana wadogo huharakisha mambo. Wanataka kujua mwisho wake ni nini.

⁷⁴ “Vema, yule nabii mkuu, baada ya kumfunulia na kumwambia hadithi ya—yake, kwamba maskini huyo mvulana mdogo alikuwa amekufa naye alikuwa amelala chumbani, sasa nabii akamwambia mtumishi wake, ‘Chukua fimbo yangu uende ukaiweke juu ya huyo mtoto.’”

Sasa, nafikiri, tena katika Agano Jipya, hapo ndipo Paulo alipopata lile wazo la kuchukua lesa na nguo kutoka mwilini mwake.

⁷⁵ “Sasa, Elisha alijua ya kwamba kila kitu alichogusa kilikuwa kimebarikiwa, lakini kama angaliweza kumfanya huyu mwanamke aamini hilo, hilo lilitosha. Kama angemfanya huyo mwanamke kuamini jambo lile lile, mwujiza ungetendeka vile vile hasa, kama mwanamke huyo angalikuwa na imani katika yale Elisha aliyomwambia afanye. Ila imani ya mwanamke huyo haikuwa kwenye hiyo fimbo.”

⁷⁶ Sasa, kidogo napenda jinsi alivyolisema, kwa vyovyote vile. “Yeye alisema, ‘Kama Bwana aishivyo na nafsi yako haifi kamwe, sitakuacha.’” Ninapenda hilo: kuyakinia kushikilia. Jambo ndilo hilo.

⁷⁷ Kama ukianza kumfuata Mungu, shikilia mpaka Roho Mtakatifu atakapokuja, mpaka kila kitu ulichooomba kimetukia. Kamwe usikate tamaa. “Sitakuacha. Mimi niko mikononi Mwako, Bwana, mpaka utakaponijibu.” Hiyo ndiyo njia ya kulifanya.

⁷⁸ Mnajua, Yesu alilifundisha hivyo. Yeye alisema hakimu dhalimu, mwajua, jinsi ambavyo a—a—asingeweza kumpa haki yule mjane kwa adui wake. Lakini yeye alisema, “Kusudi nimwondoshe mikononi mwangu nitaenda nikampe haki kwa adui zake. Vema, basi ni zaidi sana vipi Baba yako mwenye rehema wa Mbinguni atakuwa heri kukupa wewe.” Lakini sasa sio . . .

Yeye alisema, “Tafuteni nanyi mtapata; bisheni nanyi mtafunguliwa . . .” Sasa . . . “Na ombeni.”

Sasa, kama mkiangalia, sio tu [Ndugu Branham anagonga mimbara mara moja—Mh.] “Bwana, ninaitaka.”

⁷⁹ “Yeye aombaye, atafutaye.” Endelea kutafuta, endelea kubisha, endelea tu, zaidi, zaidi, umewasili hapo, kwa hiyo endelea tu kubisha mpaka litukie. “Ninaamini, Bwana. Ni—niko mikononi Mwako. Niko mikononi Mwako.”

Nakumbuka Bwana aliniponya ugonjwa wa tumbo. Ibilisi akasema, “Hu—hujapona.”

⁸⁰ Nikasema, “Kaa tu huku, nisikilize nikishuhudia basi, endapo u—unataka kuusikiliza. Endapo unataka kusikia Mungu akisifiwa, kaa tu huku ukanisikilize kwa muda kidogo.” Akachoka akaondoka. Kwa hiyo yeye—yeye atafanya hivyo.

⁸¹ Hivi majuzi alijaribu kunipa mafua mabaya. Alinipa hiyo, nami nikamrudishia. Akanipa tena. Nikamrudishia tena. Ndipo tukapigana juu ya huo kwa muda wa siku tatu ama nne, basi hatimaye ukatoweka. Kwa hiyo haya basi. Unaona? Endelea tu kumrudishia. Kamwe usiupokee, chukua, ukamrudishie. Mrudishie. Hiyo ndiyo njia ya kulifanya. Yakinia tu. Shikilia.

Hivyo ndivyo huyo mwanamke alivyofanya.

⁸² “Yeye alisema, ‘Kama Bwana aishivyo na nafsi yako kamwe haifi. . .’ Sasa, mnaona, yeye aliamini alikuwa na nafsi isiyoweza kufa. Mnaona? ‘Kama Bwana aishivyo na nafsi yako iishivyo,’ unaona, ‘sitakuacha. nitakaa pamoja nawe mpaka nipate kujua lililotukia.’ Kwa hiyo asingeweza kumwondosha mi-. . . kumwondosha mikononi mwake. Kwa hiyo ilimbidi tu kufunga viuno vyake, naye huyo hapa anaenda.

⁸³ “Ninaona wakati alipoingia chumbani, angalia yale ilimbidi nabii huyo kukabiliana nayo. Hakujua yale Bwana aliyokuwa anaenda kufanya. Huyo hapo baba, akilia kwa sauti yake yote, watu wote katika ujirani wakilia kwa nguvu. Maskini mvulana huyo mwema wa familia hii ya kupendeza alikuwa amekufa, amelazwa chumbani, matumaini yote yamekwisha.”

⁸⁴ Sasa, Elisha alifanya nini? Kama tu vile Yesu alivyofanya, akawaondosha wote nyumbani; akaondoka mahali ilipokuwa, kama vile Yesu alivyofanya wakati binti ya Yairo alipofariki. Basi tazama yale aliyofanya nabii, haikumbidi kwenda nje na kutafuta na kuomba, na kuomba sana na kujifanya tayari. La, ni—ninaamini inatupasa kudumu tumeomba kabisa wakati wote, sivyo?

⁸⁵ Hapa si muda mrefu uliopita kulikuwako na maskini mwanamke wa Kiairishi akija huku kwa meli, wao walisema. Ndipo yapata maili thelathini, arobaini huko nje, mahali fulani nje ya—ya bandari ya New York, kukaja dhoruba mbaya sana. Nayo maskini meli hiyo ndogo haikuwazia wangefaulu. Wakatuma Kilio Cha Msaada. Na kwa hiyo wakawaambia dhoruba ilikuwa ikizidi kuwa mbaya zaidi na zaidi. Kama wangeweza—kama wangeweza kuistahimili kwa dakika thelathini, wangefika ba—ba—bandarini, lakini kama wasingeweza, wangukuwa chini ya bahari. Kwa hiyo muziki wote wa jazi ulisimama na wakaanza kuomba, kucheza *Karibu Na Wewe, Mungu Wangu*, na kadhalika. Lakini maskini mwanamke huyu wa Kiairishi, yeye alitembea juu chini sakafuni akipiga mayowe na kupaza sauti. “Haleluya! Haleluya! Haleluya!” kasema.

Nahodha akasema, “Ulinielewa?”

Akasema, “Naam, bwana. Nilikuelewa.”

Kasema, “Vema, kwa nini usiombe?”

⁸⁶ Akasema, “Tayari nimeomba kutosha.” Kwa hivyo hilo—jambo ndilo hilo, omba kutosha, tayari. Hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya. Kisha akasema, “Nina furaha sana.” Ndipo akaanza kupaza sauti tena.

Nahodha akasema, “Unapiga makelele ya nini?”

Kasema, “Wewe ulisema kama tukishikilia kwa dakika thelathini tutakuwa katika New York. Kama hatukushikilia tutakuwa chini ya bahari.”

Kasema, “Hiyo ni kweli.”

⁸⁷ Kasema, “Niko njiani kutoka Ayalandi kwenda kumwona binti yangu huko New York. Nina mmoja Utukufuni. Na katika dakika thelathini kutoka sasa nitamwona mmoja wao.” Kwa hiyo hiyo ni kusema, kama hiyo meli ilizama, yeye alipaa juu, akaenda huko. Kwa hiyo jambo ndilo hilo. Huwezi kupoteza. Unaona? Kwa hiyo yeye alikuwa akipiga makelele haidhuru. Alijua katika dakika thelathini angemwona mmoja wa wapendwa wake. Loo, jambo ndilo hilo. Omba kutosha.

⁸⁸ “Maskini mzee Elisha, wakati alipoingia me—melini, ama, alipoingia jukwaani mwa mahali hapo padogo ambapo huyo mwanamke alimjengea, yeye... alitembea huku na huku sakafuni. Naye akatembea huko na huko, Biblia ilisema, chumbani. Kisha baada ya kumhisi Roho akija juu yake, alienda akajilaza juu ya mtoto huyo mchanga, naye akalala tu pale huku mwili wake ukiwa juu ya huyo mtoto mchanga. Ndipo akamhisi huyo mtoto akipata joto, kwa hiyo akasimama, akatembea huku na huko tena chumbani huku na huko. Akarudi na kujilaza juu ya huyo mtoto tena, ndipo akapiga chafya mara saba kisha akafufuka. Akamchukua huyo mtoto na kusema, ‘Mwrite Mshunami.’”

Na, loo, jinsi ambavyo maskini Bartimayo alivyoipenda hiyo.

⁸⁹ Akaanza kuwazia, “Loo, nilipokuwa nikisikia mama yangu akizisimulia hadithi hizo.” Yapata wakati huo akasikia kitu fulani kikialika, maskini nyumbu anakuja. Hapana shaka alikuwa ni tajiri, kwa kuwa karibu usafiri wote ulikuwa ni kwa miguu ama kwa... Matajiri walipanda punda, nayo majeshi yakatumia magari ya farasi. Na kwa hiyo yeye—yeye akasema, “Hapana shaka huyu ni tajiri anayekuja amechelewa.” Kwa hiyo akasimama, akatupa vazi lake kando, akakimbia nje na kusema, “Sadaka kwa kipofu; sadaka kwa kipofu, tafadhali.”

⁹⁰ Ndipo maskini yule nyumbu akasimama, ndipo akasikia sauti ya malalamishi kwelikweli ikisema, “Simile, ewe mwombaji. Mimi ni kiongozi wa shirika la wahudumu wa Yerusalem. Wananiambia kwamba kutakuwako na... Mimi ni mtumishi wa Bwana. Wananiambia wanaye mmoja wa hawa hapa wanaojiita manabii anayeshuka kuja huku leo hii, ati huona maono na kadhalika. Watafanya ibada ya uponyaji. Nitaikusanya halmashauri nzima huku chini leo. Sina budi kuwakusanya wahudumu hawa pamoja kuhakikisha kwamba hatutakuwa na upuuzi wa namna hiyo hapa. Simile, niko kwenye mapito ya Bwana.” Maskini yule punda akateremka mtaani.

Na kwa hiyo Bartimayo akawazia, “Vema, na huyo ni mtumishi wa Bwana ati.”

⁹¹ Vema, akarudi akijaribu kutafuta mahali lile jiwe lilipokuwa. Hatimaye alipolipata lile jiwe, jua lilikuwa limesogea kidogo ndipo kidogo ikawa baridi. Vivuli vya ukuta vilikuwa juu ya hilo jiwe, kwa hiyo akasogea mbali kidogo, ndipo akasema, “Vema, nadhani sina sarafu ya leo. Kwa hiyo labda nita—nitangojea kidogo tu, na labda nitaketi chini tena. Labda nitaendelea na ndoto zangu za mchana za wakati nilipokuwa mvulana mdogo.”

⁹² Ndipo akakumbuka, pia, ya kwamba mama yake alimwambia, ya kwamba miaka mingi iliyopita, ya kwamba huyo nabii mkuu Eliya na Elisha, yule aliychukua mahali pake, watu wawili wa Mungu wenye nguvu, walishuka moja kwa moja kwenye mtaa uo huo uliotandazwa mawe, wameshikana mikono, wakishuka kwenda Yordani kuufungua Yordani. Loo, jamani. Wakapita moja kwa moja yapata futi thelathini kutoka mahali alipokuwa ameketi.

⁹³ Lakini salala, kuhani alimwambia, “Siku zote za miujiza zimepita. Yehova hawaponyi watu tena, mwajua.” Roho huyo kamwe hakufa. Kwa hiyo wao, kwamba: “Loo, Yehova hafanyi mambo hayo tena. Tunapaswa tu kuishi vizuri, na—na kulipa zaka zetu, na kwenda kanisani na... kwenye kila mkutano, halafu hayo tu ndiyo tunayopaswa kufanya. Lakini Yehova haponyi. Yeye—Yeye alikuwa Yehova huko nyuma, bali siku hizi Yeye—Yeye hashughuliki nalo.”

⁹⁴ Loo, ni kosa la jinsi gani. Daima anahusika. Kama aliwahi kuhusika, angali anahusika. Naam, bwana. Hawezi kubadilisha nia Zake. Hawezi kubadilisha msimamo Wake. Angali ni Yehova. Sijali ni wangapi wanaosema ya kwamba Yeye amebadilika. Watu Wake wamebadilika, bali Yeye hajabadilika. Sababu ya sisi kutomwona akifanya mambo hayo ni kwa kuwa hatutamruhusu kuyafanya. Yeye yuko tayari.

⁹⁵ Tunafikiri tuta—tutazimaliza baraka Zake karimu. Tunafikiri, “Vema, nilimwomba Mungu anipe chakula changu cha kila siku. Sipaswi kumwomba mambo mengi kupita kiasi.” Loo, jamani.

⁹⁶ Ungeweza kuwazia? maskini samaki mdogo yapata urefu *huo*, huko mbali katikati ya bahari hii, akisema, “Ngoja, afadhali ninywe maji haya kwa unyimifu. Huenda nikaishiwa siku moja.”

⁹⁷ Ungeweza kuwazia? maskini panya mdogo yapata ukubwa *huo* chini ya yale maghala makuu ya Misri, akisema, “Afadhali nijipimie nusu punje ya ngano kwa siku. Huenda nikaishiwa kabla ya mavuno yajayo.” Jamani. Vema, hiyo ingekuwa... Ipige tu hiyo mara bilioni mia moja, nawe u—ujaribu kuumaliza wema na rehema za Mungu.

⁹⁸ Yeye anajaribu kujisukumiza ndani yako, kila awezalo. “Ombeni kwa wingi ili furaha yenu itimizwe.” Anawataka watu Wake wawe na furaha, wakiomba mambo makuu, wakiadini kwa ajili ya mambo makuu. Ninyi ni mji uliowekwa kilimani, malengo makuu, matarajio. Vema, rehema, kama tukimwona kipofu akipata kuona usiku wa leo, ninataka kuona wafu wakifufuliwa kesho usiku. Naam, bwana. Nami ninataka . . . na—naendelea tu kuadini kwa ajili ya mambo makuu.

⁹⁹ Kanisa lilipoanza kumpokea Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha, kwa nini mkakomea hapo? Jamani, endeleeni tu kusonga mbele. Nendeni kwenye nchi ya ahadi. Tuko njiani kwenda kwenye nchi ya ahadi. Hakika, usichukue tu jambo moja tu. Useme, “Vema, tutaninii tu. . . Umenena kwa lugha? Vema, huna baraka kuu mpaka utakapopata. . .” Vema, mnapaswa kuwa maili milioni moja huko barabarani kutoka hapo sasa hivi, hakika, mambo makuu zaidi; matarajio makuu. Hakika.

¹⁰⁰ Sasa, tunaona sasa ya kwamba Bartimayo alikuwa ameambiwa ya kwamba siku za miujiza zilikuwa zimepita. Kwa hiyo yeye alisema, “Sasa, vipi kama nilikuwa nimeketi hapa, badala ya kumsikiliza mtu huyo aliyejiita mwenyewe, leo hii, mtumishi wa Mungu. . . Na hayo aliyosema yalikuwa ni nini? Ati alikuwa akishuka kwenda kuona kitu fulani cha nini? Nashangaa ni kitu gani kinachoendelea huko chini mjini. Vema, kwa vyovyote vile, siku za miujiza zimepita. Na hao ndio aina ya watumishi alio nao Yehova siku hizi ati? Ni tofauti kabisa na vile Eliya alivyokuwa, na Elisha.

¹⁰¹ “Sasa, kama nilikuwa nimeketi kwenye jiwe hili, wakati Eliya na Elisha walipopitia pale chini, wakishuka kwenda Yordani. . . Na sio mbali sana chini ya pale ninapoketi ambapo nabii huyo mkuu alipovulia koti lake, joho lake, akalikunja pamoja na kuupiga Yordani, nao ukatenganika (Amina.), mamia ya miaka baada ya Yohua kufanya jambo lile lile.” Amina. Hiyo ilionyesha Yehova alikuwa angali yeye yule maadamu tu Yeye anaweza kumfanya mtu kuadini ni Yeye yule. Naam.

¹⁰² Ndipo baada ya kufika ng’ambo ya pili, sasa alikuwa amechoka. Alikuwa amegombana na Yezebeli na hao wengine mpaka. . . kuhusu kujipaka rangi na kutenda maovu, mpaka alikuwa amechoka, alikuwa anaenda Nyumbani. Na kwa hiyo huyo nabii kijana alikuwa amechukua mahali pake. Kwa hiyo alijua ya kwamba ng’ambo tu ya huo mto kulikuwako na gari la farasi limefungiwa kwenye kichaka fulani kule mahali fulani, na yeye—yeye alikuwa atafanya safari ndogo ya kwenda Nyumbani. Mnaona? Lakini huyo nabii kijana alikuwa akiingojea huduma yake mpya, akiona yale huyu mzee aliyokuwa akifanya, kwa hiyo alijua ilibidi apachukue mahali pake. Kwa hiyo huyo nabii kijana akashika ono lake, na kumwona akipaa juu, akalichukua vazi lake lililokuwa limebakishwa, akaliokota vazi lilo hilo na

kuupiga Yordani, kasema, “Yu wapi Mungu wa Eliya?” Loo, jamani. Nao ukafunguka tena. Hiyo ni kweli.

Yu wapi Mungu wa Pentekoste? Yu wapi Mungu aliyekuwa katika Yesu Kristo? Huduma ina shida gani siku hizi makanisani?

¹⁰³ Nadhani mlisoma kipande hicho cha gazeti ndio kwanza wanitumie. Mtu fulani kutoka humu kanisani alinitumia, ambapo mhudumu huyu wa Kiepiskopolia hapa juu alisema kuzaliwa na bikira kulikuwa ni hadithi ya uongo tu, wala hapakuwapo na kitu kama bustani ya Edeni, na upuuzi huo wote namna hiyo. Mtu huyo hapaswi kuwa mimbarani. La, bwana! Hiyo ndiyo shida yake siku hizi. Hiyo ndiyo. . . Wanawachukua watu wenye elimu namna hiyo kusimama nao wanapata elimu nyingi sana hawana ujasiri wa kutosha kujua jinsi ya kuishikilia. Hivyo tu.

¹⁰⁴ Tunachohitaji leo hii. . . Paulo alisema, “Sikuja kwenu kwa maneno ya ufasaha ama elimu. Nilikuja kwenu kwa unyenyekevu pamoja na nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu, ili kwamba imani yenu itulie juu ya kufufuka na nguvu za Mungu, wala sio katika maneno laini,” ama kitu fulani cha anayejiita askofu, ama kitu fulani.

¹⁰⁵ Sasa, tunaona ya kwamba muda mfupi tu baadaye, wakati Bartimayo akiketi pale muda kidogo zaidi, akishangaa kile kingetukia. Ndipo akakumbuka ya kwamba, pia, chini tu ya mahali pale, sio yadi mia tano kutoka mahali alipokuwa ameketi, Yoshua yule mkuu, loo, jamani, mtumishi huyo mashuhuri wa Mungu ambaye alipachukua mahali pa Musa, ambaye alipitia kwenye Bahari ya Shamu, na akavuka, pia alikuwa tu wa yale makundi mawili ya kale nyikani huko nyuma walioamini ya kwamba wangeweza kuiteka ile nchi. Waliliangalia Neno la Mungu. Waliliamini Neno la Mungu.

¹⁰⁶ Tisa kati yao walisema, “Loo, hatuwezi kuiteka. Sisi tunaonekana kama nzige karibu nao. Miji yote imezingirwa na kuta. Haiwezekani kuiteka.”

Lakini sio jamaa huyo, la, bwana, ndugu, yeye alisema, “Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka.”

¹⁰⁷ Mbona? Inategemea kile unachoangalia. Kama unaungalia mkono wako uliolemaa, ninii tu, ungali utakaa hivyo. Kama unaangalia uvimbe wako, utabaki hivyo. Usiangalie hayo. Iangalie ahadi ya Mungu. Inategemea kile unachoangalia. Wakristo huangalia yasiyoonekana. Ibrahimu aliyaita mambo yasiyokuwapo kana kwamba yalikuwapo, kwa kuwa Mungu alisema yalikuwa. Hivyo ndivyo Wakristo halisi wafanyavyo. Haidhuru ulimwengu unasema nini, jinsi unavyoonekana, hilo halina uhusiano wowote nalo. Yale Mungu aliyosema kulihusu ndiyo muhimu. Naam. Kilichokuwa. . .

108 Mungu aliwaambia huko chini kabisa Misri, “Nimewapa nchi hiyo.” Bali Yeye hakusema, “Nitaenda huko nje na kuwafagilia mbali, na kuzipamba nyumba, na kuweka mapazia, na kila kitu. Nyote mwingie tu.” La, la. Iliwabidi kupigania kila inchi ya ardhi waliyoiteka. Hiyo ni kweli, kupiga vita, na kuiteka kwa kila... kupiga vita kila inchi. Bali Yeye alisema, “Kila mahali nyayo za miguu yenu zitakapokanyaga, huo ni umiliki.” Nyayo za miguu ni umiliki.

109 Hilo ndilo jambo lile lile siku hizi. Uponyaji wa Kiungu ni wetu. Roho Mtakatifu ni wetu. Ni mali yetu, bali itakubidi kupigania kila inchi yake. Naam, bwana. Lakini ndugu, nyayo za miguu ni umiliki. Endelea tu kupiga vita. Iteke. Ibilisi anasema, “Siku za miujiza zimepita.”

110 Sema, “Unadanganya. Mungu alisema Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.” Iteke. Kila mahali mguu wako utakapokanyaga, huo ni umiliki. Hiyo ni kweli.

111 Yoshua alivuka moja kwa moja mtoni pamoja nao, akapiga kambi huko nje. Loo, kipofu Bartimayo akasema, “Vipi kama ningaliishi katika siku hizo? Mbona, mara nilipowaona hao makuhani wakitembea, naye Yoshua pamoja na ule upanga hewani, akivuka, mbona, ningalishuka kule na kusema, ‘Yoshua mkuu, niombe.’ Nami ninaamini ningalipata kuona, mtu huyo mkuu angaliniombea. Hakika. Bali ole, Yoshua ameondoka, naye Mungu, nadhani, ameondoka. Siku zote za miujiza zimepita, ndivyo kuhani wetu anavyosema. Kwa hiyo nadhani hamna matumaini. Hakuna kitu ninachoweza kufanya; kwa hiyo, hakuna matumaini.”

112 Ndipo basi akasema, “Mnajua nini? Wakiisha kuzingira kuta za Yerusalemu siku nyingi, siku moja Yoshua, yule shujaa mkuu, alikuwa akitembea huko nje kidogo alasiri moja, akichunguza mikakati ya jinsi ya kuziteka hizo kuta za Yeriko, jinsi atakavyofanya hivyo. Aliona ule uzi mwekundu wa Rahabu ukining’inia chini. Yeye alikuwa anaenda kuihifadhi nyumba hiyo, akiangalia. Ndipo mara akaangalia, akisimama hapo mbele zake, alisimama Mtu amechomoa upanga Wake. Yoshua akachomoa upanga wake, akakimbia kumkabili Yeye, akampa changamoto wapigane hao wawili. Akasema, ‘Uko upande wetu, ama uko upande wa adui yetu?’

113 “Yeye akasema, ‘Mimi ni jemadari wa jeshi la Bwana. Mimi ndimi Jemadari wa Bwana wa jeshi Lake.’ Yoshua akatupa chini upanga wake, akavua helmeti yake, akaanguka miguuni Pake.”

114 Bartimayo kipofu angalisema, “Loo, kama ningaliishi katika siku hizo, ningalikimbia kwa Jemadari huyo wa Bwana wa majeshi, nami ningalizungumza Naye.”

115 Hakujua hata kidogo ya kwamba Jemadari yuyo huyo hakuwa yadi mia moja kutoka kwake, akija moja kwa moja

kupitia mjini wakati huo, Jemadari wa jeshi la Bwana akienda Zake kupitia mjini.

¹¹⁶ Mnajua, ni wakati tunapoanza kuwazia juu Yake, hapo ndipo Yeye anapotokea. Ni wakati Kleopa na hao wengine walipokuwa wakizungumza juu Yake, ndipo alipotokea. Sikuzote ni wakati... “Jalia tafakari za moyo wangu na—na yajalie mawazo yangu yote, na ujalie nyimbo zangu zote, jalia yote niliyo yatafakari tu juu Yako, Bwana, usiku na mchana.” Hiyo ndiyo njia ya kumleta Mungu karibu nawe.

¹¹⁷ Acha kuwazia yale akina Jones wanayofanya, na yale utakayofanya juma lijalo, na jambo hili lote. Weka tu...acha tu... “Ijaze njia yangu kila siku na upendo ninapotembea pamoja na Hua wa Mbinguni. Jalia niende wakati wote pamoja na wimbo na tabasamu. Ijaze njia yangu kila siku na upendo.” Hiyo ni kweli.

¹¹⁸ Shuka moja kwa moja barabarani haidhuru nini; shule inaweka, ama la. Kama haiweki, tumfukuze mwalimu, na kuendelea moja kwa moja tukimwamini Bwana. Mnaona? Weka tafakari juu ya Mungu. Wazieni mambo haya. Biblia ilisema, “Zikiwepo sifa zozote, kukiwako na staha yoyote, yatafakarini mambo haya.”

¹¹⁹ Vema, mawazo yetu sikuzote ni mabaya. Tunakuja kwenye mstari wa maombi...ninaona wanaingia katika mstari wa maombi, “Loo, kama—kama—kama yeye ataniambia...Ni *huu?*” Loo, jamani, kamwe hupati kitu jinsi hiyo. La. Wewe ni kinyume sana kwanza.

¹²⁰ Njoni namna hiyo: “Njoni kwenye chemchemi iliyojaa Damu iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambapo wenye dhambi wanapotumbukizwa chini ya hiyo gharika hupoteza doa lao lote la hatia.” Jambo ndilo hilo. Njoni kwa imani mkiamini. “Yeye amjiaye Mungu hana budi kuamini ya kwamba Yeye yuko, na Mtoa thawabu kwa wale wamtafutao kwa bidii.”

¹²¹ Sitapitia kwenye mstari wa maombi wa Oral Roberts, kisha nipitie kwenye mstari wa maombi wa Tommy Hicks, kisha nipitie kwenye mstari wa maombi wa Osborn, na mstari wa maombi wa Allen, na mstari wa maombi wa Branham, mstari wa maombi wa *Fulani-wa-fulani*, niende kwenye kanisa *hili* na kanisa *lile*. Mbona, unapoteza tu wakati; hivyo tu. Hivyo tu.

¹²² Jambo la kufanya ni ku—kusema tu na kuamua ya kwamba ni Mungu, na Mungu alisema hivyo, nami nitatimiza masharti Yake na hilo linalitatu milele. Amina. Jambo ndilo hilo. Mungu alisema hivyo. Niende kwa mchungaji wangu, niseme, “Mchungaji, Biblia inatwambia kuwaita wazee, kuwapaka mafuta, kuwaombea, maombi ya imani yatamwoko mgonjwa huyo. Hayo tu ndiyo yanipasayo kujua.” Amina.

¹²³ Nilipata barua kutoka kwa maskini mwanamke mmoja kutoka Ujerumani sio muda mrefu uliopita. Mbona, alikuwa

amelemaa kwa muda wa miaka kumi na mitano kwa yabisi kavu: asingeweza kusogea. Nikamtumia lesa. Sisi hutuma maelfu yake, kwa mwezi, nje. Na kwa hiyo, akapata barua hii ndogo. Nasi tuna maombi ya pamoja kote ulimwenguni. Kwa hiyo yeye—yeye akaisoma hii, ndipo akasema, “Sasa, inasema hapa, ‘Kama mchungaji wako hayupo, ama kama yeye ni asiyeamini, usimwite. Mnaona? Lakini endapo kuna jirani mahali fulani ambaye ni mwaminio, mwite mwaminio huyo. Kiri makosa yako yote. Mwombe Mungu akusamehe kila kitu ulichofanya. Fanya kila kitu sawa. Kisha omba. Weka hii lesa chini ya vazi lako moyoni mwako. Kisha uamini.’” Kwa hiyo alitimiza masharti yote aliyotumiwa. Basi alipofanya hivyo, aliuweka mkono wake juu ya moyo wake. Akasema, “Sasa, ewe mzee ibilisi, umekuwa ndani yangu muda mrefu kutosha. Toka.” Huyu hapa anakuja akitembea. Hiyo ni rahisi tu hivyo. Ni rahisi hivyo tu kuamini.

¹²⁴ Hapa Arizona, tulikuwa huko kwa Wahindi, Waapache. Na sikuzote niliwasikitikia Waapache. Nao walikuwa hapo nje usiku huo. Na ilionekana kama jeshi lililoketi huko nje, nami nikaanza kuwazungumzia kuhusu Bwana. Nanyi mwajua, Mhindi, kwa namna fulani yeye ni jamaa wa kipekee. Yeye ni kama nyumbu: hatakula katika zizi lingine. Kwa hiyo akausikiliza, alidhani ulikuwa ni wa bandia, kwanza. Ndipo akaleta... Nikasema... Nikafanyiza mstari wa maombi.

¹²⁵ Vema, nikasikia mtu fulani huko nje akipiga makelele “Gloria a Dios.” Hao walikuwa ni marafiki wangu Wahispania. Nilijua wangukuwa na mstari wa maombi kama walikuwa karibu, maana wao ni... sikuzote wana imani ya kuamini. Kwa hiyo walikuwa... bali wao... huu ulikuwa ni kwa ajili ya Wahindi peke yao.

¹²⁶ Nami nikaangalia kote kule, na jambo la kwanza, yule mwanamke wa Assembly of God kule nyuma, alikuwa na misheni ndogo. Nilikuwa nimesimama juu kwenye—kwenye vipandio namna *hii*, na wote walikuwa wameketi kuzunguka. Yalikuwa ni mandhari mazuri. Na kwa hiyo alikuwa na wengine ndani huko nyuma. Wakamtoa mwanamke wa kwanza. Mara alipojitokeza, vifundo vikubwa sana vya mikono, vipana, alikuwa na mtoto mchanga mgongoni mwake, katika mbeleko huu mdogo hapa nyuma. Nami nikamwangukia. Ndipo nikawazia ningejaribu kupata kibali. Nikasema, “Vipi kuhusu kunipa mimi huyu mtoto?” Hakutaka kufanya hivyo. Kwa hiyo mimi, nikiishika tu nia yake.

¹²⁷ Sasa, nikasema, “Sasa...” Kwa mkalimani, nikasema, “yeye ana ugonjwa wa zinaa, bali ni...” Basi mkalimani akasema hivyo. Akanikodolea macho sana. Nikasema, “Sasa, haukusababishwa na maisha ya utovu wa uadilifu, bali ni kwa jinsi ilimbidi kuishi katika uchafu na kinyaa namna hiyo.” Vema, akakitikisa kichwa chake hiyo ilikuwa ni kweli; nikamwombea.

¹²⁸ Aliyefuata alikuwa na glakoma ya jicho. Wahindi wanayo kwa wingi, basi nikamwomba huyo. Mwingine aliyetoka alikuwa ni—alikuwa ni msichana mdogo, naye alikiinamisha kichwa chake namna *hiyo*. Nikasema, “Sasa...” Alikuwa ni jamaa mdogo karibu *hivyo*. Basi ilitokea kwamba alikuwa mmoja wa binti za chifu. Nikasema, “Sasa, huyu msichana mdogo,” Nikasema, “amekuwa na homa, nayo hiyo homa ikamfanya kuwa kiziwi na bubu. Hawezi kuzungumza wala kusikia.”

¹²⁹ Ndipo mkalimani akasema hivyo, na mama, “Hiyo ilikuwa ni kweli, kila sehemu yake ilikuwa ni kweli.” Hao Wahindi wakaanza basi kuangaliana, mwajua. Wakaanza kuona kitu fulani hawakuwa wamekiona kamwe. Naam.

¹³⁰ Kwa hiyo nikasema, “Sasa, siwezi kumfanya hu—huyu msichana kuzungumza na kusikia. Inamhitaji Mungu.” Lakini nikasema, “Hii ni—ni ishara tu ya kwamba Yeye yupo hapa, kwamba Uwepo Wake upo hapa. Ametupaka mafuta.” Na kwa hiyo nikamshika mkono maskini msichana huyo mdogo. Nikasema, “Baba wa Mbinguni.” Wao hawatafsiri maombi. Nikasema, “Jalia pepo huyu kiziwi na bubu amwache mtoto huyu.” Ndipo nikamfikia, nami nikafanya *hivyo*. [Ndugu Branham anapiga makofi yake—Mh.] Akageuka na kuniangalia mimi kwa macho hayo makubwa meusi, nami nikasema, “Wewe sema, ‘Bwana asifiwe.’”

Akasema, “Lum, lum lumalum,” ama kitu kingine, namna hiyo.

Nikasema, “Atazungumza vizuri zaidi.”

Mama yake akasema, “Mazungumzo yake yanakuja vizuri sasa hivi.” Na—naye huyo akaenda; kwa hiyo basi, “Mazungumzo yake yanakuja vizuri sasa hivi.”

¹³¹ Ndipo aliyefuata alikuwa ni mama, kisha mwingine alikuwa ni maskini mvulana mdogo aliyekuja huko nje. Nami nikasema, “Vema, unaamini ya kwamba Mungu... Unazungumza Kiingereza?” La, hakuzungumza Kiingereza. Nikasema, “Unaamini ya kwamba Mungu atamponya maskini jamaa huyo mdogo?”

¹³² Ndipo akanyosha mkono chini na kumshika juu ya kichwa; wao wana fujo kweli, mwajua, nazo maskini nywele zake zinakwaruza kama manyoya ya shingoni mwa farasi, na kwa hiyo... kumshika namna *hiyo*. Nikasema, “Yeye ana makengeza, lakini unaamini ya kwamba Mungu...?” Akamsikia mfasiri akisema, “makengeza,” kwa hiyo akamshika juu ya kichwa, na kukivuta maskini kichwa chake nyuma, macho yake madogo yamekaa namna *hiyo*. Nikasema, “Sasa, kama utaamini ya kwamba Mungu atayanyosha macho yake madogo,” nikasema, “basi Mungu atafanya hivyo.” Ndipo mfasiri... Nikasema, “Sasa, enda polepole.”

¹³³ Hawana se—sentensi yoyote wala vituo. Wanaanza polepole sana, kisha wanapanda juu, juu, chini. Wananinii tu... Mnajua jinsi Waapache walivyo. Wao ni...walikuwa kidogo ni kundi kali la Wahindi. Kwa hiyo basi wakasema, “Naam,” kwamba angeamini.

¹³⁴ Nikamchukua jamaa huyo mdogo juu kwa... Yeye alikuwa tu kama kwamba unajaribu kumfunza farasi asiyefunzwa utii. Nami nilikuwa na kipande cha chingamu. Nikaiweka chini ya pua yake na kumwacha ainuse, mwajua. Halafu nikamweka *hivi*, nikamshika mikononi mwangu, nikamweka huyo jamaa mdogo mikononi mwangu namna *hii*. Nikasema, “Usifasiri hili.” Nikasema, “Baba wa Mbinguni, watu hawa maskini, hawa ndio Wamarekani halisi kweli.”

¹³⁵ Na hiyo ni kweli. Sisi si Wamarekani. Huh-uh. Sisi si Wamarekani. Sisi ni wageni walioingia, tukawanyang’anya nchi. Wao ndio Wamarekani halisi. Mungu aliwapa nchi *hii*; sisi tukaja, tukawanyang’anya. Nafikiri ni doa kwenye bendera jinsi tunavyowatendea. Hiyo ni kweli. Kutuma pesa huko Japani na mahali hapo pote, kutulipulia tena namna *hii*, nao Wahindi wetu wamekaa huku nje wakifa kwa njaa, sio haki. Hakika, si haki.

¹³⁶ Ndipo basi nikaangalia, na maskini jamaa huyo, nilikuwa nimembeba begani mwangu. Nikasema, “Bwana, jalia nipate kibali kwa watu hawa. Yanyoshe macho ya maskini jamaa huyu.” Nilikuwa nikiangalia namna *hii*, nami nikaona ono mbele yangu, macho yake madogo yalikuwa yamenyoka kabisa.

¹³⁷ Nikasema. “Sasa...” Alikuwa ameweka kichwa chake begani mwangu. Nilikuwa nikimpapasa. Nikasema, “Sasa, kwenu nyote,” mamia na mamia wameketi kila mahali, nikasema, “sasa, kama macho ya mtoto huyu mchanga hayajanyoka, basi mimi ni nabii wa uongo. Mnaona? Kama yakinyoka, basi nimemwakilisha Yesu Kristo kwenu. Siwezi kusaidia yale serikali inayowafanyia. Lakini,” nikasema, “najua Yesu atawatendea haki. Sasa, mtaona kama hili ni kweli ama si kweli.” Nikakigeuza maskini kichwa chake. Nena kuhusu mstari wa maombi. Nilikuwa na mmoja sasa. Jamani, kulikuwako na mkanyagano.

¹³⁸ Kisha aliyefuata alikuwa ni mwanamke Mhindi mkongwe, naye alikuwa na...Alikuwa ndiye angefuata na, loo, walikuwa...unaninii tu...ilikubidi tu...Usingeweza kuwazuia. Basi kulikuwako na—kulikuwako na mwanamke mkongwe wa Kihindi aliyejitokeza. Alikuwa na mipini miwili ya ufagio pamoja na—pamoja na kipande cha kitambaa kimezungushiwa kitu fulani kilichokuwa chini ya mkono wake *hapa*, naye alikuwa akijaribu kutoka.

¹³⁹ Ndipo kulikuwako na mvulana mdogo wa Kihindi aliyeruka pale, naye alikuwa akijaribu kuruka aingie mbele yake. Wala tusingeweza kumfanya aelewe, maana asingeweza kuzungumza

Kiingereza. Ndipo Ndugu Moore, wengi wenu mnamfahamu Ndugu Jack Moore; alimshika tu ubavuni, akambeba huko.

¹⁴⁰ Nami nikamwona huyo mwanamke mkongwe. Akajongea karibu namna *hiyo*. Walikuwa wakiamini wakati huo. Loo, nena kuhusu mstari wa maombi. Kwa hiyo hapo, wakija tu, kabisa, namna *hiyo*. Basi nikamwangalia, naye alikuwa akiisogeza hiyo mikongojo miwili namna *hii*. Naye angeuchukua mguu huo, mwajua, na kuuweka nje, halafu huo mwingine namna *hiyo*, angejongea tu kwa shida sana. Yeye, nadhani, alikuwa na umri wa miaka themanini. Ndipo akaniangalia mimi wakati alipofika karibu sana nami. Na hiyo mikato mikubwa mno, yenye kilindi shavuni mwake. Mama yangu ni chotara, sijui kama mnajua hilo ama la, lakini yeye ana hiyo mikato mikubwa mno, yenye kilindi, pia. Nikaangalia wakati alipokuja namna *hiyo*, huku machozi yakitiririka kupitia kwenye macho hayo madogo, yaliyoonekana yamekwajuka. Ndipo nikawazia, “Mama ya mtu fulani.” Naye akaniangalia tu namna *hiyo* ndipo nikawazia, mimi—mimi... wakati mimi... kabla sijamwombea, nikawazia, “Ee Mungu, angalia maskini kidevu hicho kikitikisika namna *hiyo*, maskini mkongwe.” Akaniangalia, akaanza kutabasamu. Akachukua tu mikongojo mmoja na kuuweka *pale*, kisha akanikabidhi, kisha akaondoka akitembea jukwaani. Naam. Mnaona, imani rahisi, kuamini tu.

¹⁴¹ Ni—nilikuwa nikienda kujaribu kuwaombea wote, lakini, loo, jamani, ilikuwa ni karibu... Ilinibidi kukomesha upambanuzi basi. Kwa hiyo yapata saa tisa ama kumi usiku, walikuwa wakipitia pale wamelowa maji, kote kote huko namna *hii*, wamelowa maji tu walivyoweza kuwa. Ndipo nikasema, “Kwani imekuwaje kwao?”

¹⁴² Kasema, “Vema, walidhani, kwanza, wewe ulikuwa mwongo.” Yeye akasema, “Sasa,” kasema, “wanaenda huko jangwani na kuwachukua wapendwa wao. Hawashuki kwenda kwenye kivuko cha maji mafupi; wanapitia moja kwa moja mtoni kwa shida pamoja nao, namna hiyo.”

¹⁴³ Basi huyu hapa mzee anakuja, mwenye mvi. Naye alikuwa na... alikuwa juu ya ubao nao ulikuwa na vijiti viwili vimeukingama. Naye alikuwa ameweka miguu yake juu ya vijiti viwili na mikono yake imekingama vijiti viwili, naye alikuwa akitetemeka hivi kwa ugonjwa wa kupooza. Na kwa hiyo kulikuwako na jamaa mkubwa mno amesimama pale, mwenye sura nzuri, Mhindi mkubwa mno, midomo yake ni samawati iwezavyo kuwa, na amelowa maji. Ndipo nikasema, “Hivi huogopi utashikwa na nimonia?”

Akasema, “La.”

Nikasema, “Unazungumza Kiingereza?”

Kasema, “Kidogo.”

Nami nikasema, “Wewe huogopi utashikwa na nimonia.”

“La.” Kasema, “Yesu Kristo amenishughulikia. Nilimleta baba yangu.”

“Hum, um-hum, um-hum.” Nikasema, “Huyo ni ndugu yako?”

“Naam.”

Nikasema, “Kama nikimwombea, unafikiri atapata afya?”

“Naam.”

“Yeye huzungumza Kiingereza hata kidogo?”

“La.”

Nikasema, “Mpishe hapa.”

¹⁴⁴ Wakampisha. Nikaweka mikono yangu juu yake, maskini kichwa chake kikitikisika namna *hiyo*. Nikasema, “Baba, yeye alifanya kazi siku nyingi sana kwa ajili ya wavulana hawa. Wamemheshimu sasa, wakimvusha mtoni usiku namna hii apate kuombewa. Ninaomba ya kwamba Wewe utamponya.” Nikasema, “Mchukueni. Mleteni anayefuata.”

¹⁴⁵ Muda si muda mwajua, nilisikia kila mtu akipiga makelele, mayowe. Nikaangalia, yule mzee alikuwa ameubeba ule ubao mgongoni mwake, akizunguka-zunguka akimpungia kila mtu mkono, namna hiyo, akiondoka. Hivyo ndivyo ilivyo. Ni imani rahisi tu kumwamini Mungu. Sio udanganyifu. Ni imani tu kama ya mtoto. Mnaona, tu—tumeruka mbali moja kwa moja tukaachana na kujaribu kuielezea. Amini tu.

¹⁴⁶ Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo ilivyo na huyu Jemadari mkuu, mwenye nguvu wa jeshi la Bwana, Alikuwa hapo usiku huo, kama vile alivyokuwa pale. Nanyi mwajua, kuna jambo moja ama lingine kulihusu, mahali Yesu alipo, sikuzote unasikia kelele nyingi sana. Sijui ni kwa nini, bali ni—ndivyo ilivyo. Popote unapomwona Yesu unakuta kelele nyingi.

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... wakisukumana na kupiga makelele, na baadhi yao wikipayuka jambo moja kwa sauti kuu, “Hosana, Hosana, kwa Nabii wa Galilaya.”

¹⁴⁷ Wengine wakisema, “Mwondoleeni mbali huyo laghai. Mwondoeni kwenye mji huu. Hatumtaki hapa.” Na wengine wakimtupia tunda lililooza, na labda mayai vivyo hivyo, mwajua, kisha kuendelea.

¹⁴⁸ Naye akasema, “Ni nani anayepitia hapa?” kasema Bartimayo. “Ni nani anayepita?” Nao wakamzunguka, na kumsukuma nyuma na labda baada ya kitambo kidogo yeye... wakamwangusha chini. Akaketi chini, akaligusa jiwe lake tena. Watu... angemsikia mtu fulani akisema, mmoja alikuwa upande Wake, mwingine anampinga. Ndivyo ilivyo siku hizi: wengine wako upande Wake, wengine wanampinga.

¹⁴⁹ Mara akamsikia kuhani yule aliyekuwa amemsikia akiingia, akisema, “Hei, wewe, nabii, wewe, wewe uliyesema ulimfufua

mtu aliyekufa jina lake Lazaro; tunayo makaburi yaliyojaa wao hapa juu. Hebu tukuone ukikwea na kumfufua mmoja. Tutakuamini. Mpaka utakapofanya hivyo, wewe ni nabii wa uongo.”

Akasema, “Huyo ni mtu yule yule aliyeniambia anashuka kwenda kukomesha...Vema, hayo yote yanahusu nini?” Mnaona?

¹⁵⁰ Naye angesema, “Hebu mtu fulani aniambie. Mtu anisaidie. Mtu anisaidie, kwa sababu...Mbona...? Ni nani anayepitia hapa? Makelele haya yote yanahusu nini?” Hakuna mtu angalimsikiliza, basi baada ya kitambo kidogo, hapana shaka ilikuwa ni msichana. Alimwona maskini huyo jamaa mzee amelala pale, naye akamsimamisha. Akasema, “Bwana, umeumia?”

“La, mama.” Akasema, “La—laiti ungaliniambia, haya makelele yote yanahusu nini?”

“Loo,” akasema, “Yesu wa Nazareti anapitia hapa.”

“Mbona, Yesu wa Nazareti ni Nani?”

“Kwani wewe si Mwisraeli?”

“Naam.”

¹⁵¹ “Vema, unaona, mimi ni mtumishi wa Yesu wa Nazareti.” Mnajua kuna jambo fulani kuhusu mtumishi wa Yesu wa Nazareti; wao daima wako tayari kumsaidia mtu aliye mhitaji. Sikuzote wako tayari kusimama na kumsaidia mtu aliye mhitaji. Watumishi wa Mungu hufanya hivyo. Akasema, “Mimi ni mwaminio wa Yesu wa Nazareti. Sasa, wajua, Yesu huyu wa Nazareti ni Mwana wa Daudi, ambaye...”

“Ati Mwana wa Daudi? Mbona, ninakumbuka...Nilikuwa tu nimeketi hapa nikiwazia, na mama yangu aliniambia ya kwamba Mwana wa Daudi angekuja siku moja.”

“Naam, huyo Ndiye, yule Nabii wa Galilaya.”

“Ati Nabii?”

“Naam.”

Kasema, “Unamkumbuka mtu yule hapa chini mjini wanayemwita Zakayo, mfanyabiashara?”

“Naam, ninamkumbuka vizuri sana. Uh-huh, amenipa mimi hela hapo kabla.”

“Vema, asubuhi ya leo...Unamjua Rebekah, mkewe?”

“Naam, ninamkumbuka Rebekah.”

¹⁵² “Vema, Rebekah amekuwa akiomba. Akijua ya kwamba Yesu alikuwa akija mjini, mbona, alikuwa akiomba ya kwamba—kwamba mumewe angempo...angempokea Yeye kama Mwokozi wake.”

“Naam, endelea, endelea kuzungumza.”

153 “Vema, asubuhi ya leo, Zakayo alikuwa akitoka kwenda kumwona, wala hakutaka Yesu amwone. Kwa hiyo akashuka mbio pembeni mwa Barabara Kuu ya Haleluya ambapo inapiga kona kwenye Barabara ya Utukufu hapa chini, naye a—akachukua mtungi wa takataka na kuuweka chini, kisha akapanda juu ya mkuyu, akaketi chini mahali matawi mawili yanapokingama.”

“Uh-huh.”

154 “Naye Rebekah alimwambia ya kwamba—ya kwamba, ‘Sasa, wewe ni Myahudi, nawe unajua ya kwamba atakapokuja Masihi, Yeye atakuwa ni Nabii. Atakuwa ni Mungu-Nabii, maana Musa alisema, “Bwana Mungu wako atamwinua Nabii aliye kama nilivyo mimi.”’ Lakini unajua, u—unamjua Zakayo, vile hasa . . . yeye—yeye ni mmoja wa wafanyabiashara hapa mjini. Naye anaegemea sana pamoja na . . . Yeye na rabi hucheza karata pamoja, nao wana ninii yao, unajua, ninii ya—yao kwenye . . . mambo ni sawa kabisa. Kwa hiyo wao, rabi na hao wote wamesema jamaa huyo asiaminiwe, maana yeye hakuwa nabii.

155 “Kwa hiyo Zakayo alitaka kuona kama Yeye alikuwa. Kwa hiyo anapanda mti huu, naye akachukua matawi yote, kisha akayavuruta yote kumzunguka *hivi*, akajifunika nayo. Naye alikuwa na jani moja kubwa la mtende aliloliinua juu apate kumwona wakati alipopiga kona pale kwenye Barabara ya Utukufu, wajua, kumwona akikaribia. Kwa hiyo akaketi hapa juu ya mti, amekaa juu kabisa, wala hakuna mtu aliyejua alikuwa huko juu. Naye akasema, ‘Sasa, nitaona kama Yeye ni Nabii. Nami nitamwalia usoni Mwake, nitajua kama Yeye ni Nabii ama siye. Ninajua jinsi nabii anavyopaswa kuonekana.’

156 “Nao wanafunzi wote wakatokea kwenye kona. Naye huyu hapa yule mvua samaki mkubwa anakuja, akisema, ‘Mwaweza kurudi nyuma, tafadhali? Bwana wetu amechoka sana. Tuna—tunasikitika inatubidi kufanya jambo hili, bali mwaweza kurudi nyuma tu kwa dakika moja mumwache apite? Yeye anaenda kwa Levinski kwa ajili ya chakula cha kutwa, kwa hiyo itawabidi kuninii . . . kwenye ule mkahawa hapa juu, mnaona, kwa hiyo ita—itawabidi kurudi nyuma. Nasikitika inatulazimu kufanya jambo hili, lakini . . .’” Hakika, natumaini hakuna Levinski hapa. Kwa hiyo basi, kwa vyovyote vile, nilimaanisha tu . . . Niliwaambia ilikuwa ni mchezo wa kuigiza tu. “Kwa hiyo kupitia pale na kuwaambia, mwajua, ‘Rudini nyuma kidogo tu.’ Nao hawa hapa wengine wanakuja.

157 “Naye a—akainua jani lake na kuangalia nje. Akasema, ‘Um-hum. Akina nani wale? Loo, loo, hao wanapaswa kuwa ni wanafunzi Wake Rebekah alioniambia habari zao. Um-hum, nitangojea kwa dakika moja tu.’ Ndipo baada ya kitambo kidogo akaliinua lile jani tena, kasema, ‘Sasa, hebu tuone kama nimefunikwa vizuri. Naam, nimeketi kwenye matawi mawili.’”

Hapo ndipo njia mbili zinapokutana, na hapo ndipo watu wengi huketi, ambapo njia yako na ya Mungu hukutana. Hiyo ni kweli, huna budi kufanya uamuzi kutoka papo hapo.

¹⁵⁸ “Kwa hiyo a—alikuwa ameketi kwenye tawi hili, mwajua. Naye akaangalia, na baada ya kitambo kidogo kwa namna fulani akaona mahali patupu, ndipo baada ya kitambo kidogo akaangalia, wakipiga kona. Akaliinua jani lake polepole na kuangalia nje, akachungulia kutoka chini ya pembe lake. Nanyi mwajua nini? Akamwangalia Yeye usoni. Na mara alipomwona kwa uso, yeye alisema, ‘Kuna kitu fulani tofauti kidogo kumhusu Mtu huyo. Ninaweza kumsikia jinsi alivyozungumza, na jinsi alivyokuwa na huruma, Yeye—Yeye alikuwa ni tofauti. Lakini mnajua ingenibidi kujua ya kwamba Yeye alikuwa ni Nabii, kwa sababu kama Yeye si Nabii basi Yeye siye Masihi, kwa sababu Musa alitwambia ya kwamba huyo Masihi angekuwa ni Nabii.

¹⁵⁹ “Kwa hiyo nimempumbaza sasa. Nimemwangalia vizuri. Ninarudi kumwambia Rebekah. Mnajua lile ninalowazia vizuri kufanya? Kuruka kutoka kwenye mti huu na kumkemea kwelikweli.” Mnajua—mnajua jinsi watu, mwajua. “Ninaamini nitamwambia ya kwamba siku zote za miujiza zimepita, maana Levinski alisema hivyo, na hao wengine wote. Rabi Jones na hao wote walisema hivyo.” Mnaona? “Kwa hiyo mimi ninajua; ninaamini nitafanya hilo. Lakini afadhali nitulie, maana nimejifunika vizuri sana.’

“Kwa hiyo akatembea . . .” kasema, “na—na jina lako ni nani, bwana?”

“Mimi ni Bartimayo.”

¹⁶⁰ “Vema, Bartimayo, Yeye alitembea mpaka akafika moja kwa moja chini ya mti. Ndipo wakati alipofika chini ya mti akasimama, akaangalia juu, kasema, ‘Zakayo, shuka mara moja. Ninaenda nyumbani pamoja nawe kwa ajili ya chakula cha kutwa.’ Zak-. . . Bartimayo, ungeamini huyo alikuwa ni Mwana wa Daudi?”

“Loo, naam. Hivyo ndivyo Yeye atakavyofanya. Yuko wapi?”

“Tayari amefika mbali sana kule barabarani sasa.”

¹⁶¹ Akaruka juu na kulitupa koti lake chini. “Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu. Unirehemu. Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu. Naam, unirehemu.” Nafasi yake ya mwisho, huyo hapo akipita, tayari alikuwa amepita, basi angewezae kamwe kumsikia maskini mzee huyo kipofu, asiye na maana?

Nao watu wakasema, “Keti chini, keti chini. U—usiwe ukipiga mayowe namna hiyo. Ketu chini. Yeye ameshuka barabarani.”

¹⁶² Ndipo hapana shaka ilikuwa ni kwamba Bartimayo alisema, “Yeye ni Masihi, ninajua Ndiye. Jinsi pekee nitakavyoweza

kumshika sasa, kama Yeye yuko huko chini, ninajua ya kwamba Masihi, ajapo, Yeye atatwambia mambo yote, tunajua ya kwamba Yeye atakuwa ni Nabii.” Kwa hiyo hapana shaka alianguka magotini mwake na kusema, “Yehova Mungu, kama huyo ndiye Masihi, huyo ni Mwanao. Ninaomba ya kwamba Wewe utamsimamisha. Loo, jalia anirehemu.”

Ndipo Yesu akasimama. Ilikuwa ni kitu gani? Si sauti yake iliyomsimamisha, bali imani yake ilimsimamisha. Angalieni, “Imani yako imekuokoa.” Mnaona?

¹⁶³ Angalieni. Pamoja na mizigo yote ya ulimwengu, Yeye alikuwa akienda moja kwa moja Yerusalemu kusulubiwa; Yeye alijua hivyo. Mizigo yote na dhambi za ulimwengu: kila dhambi iliyopata kutendwa, ama itakayopata kutendwa, ilikuwa juu Yake. Wazieni, moyoni Mwake; hata mayai na matunda na kadhalika alitupiwa, makelele yote ya “Njoo huku ukawafufue wafu. Utuonyeshe mwujiza. Hebu tukuone ukifanya *hivi-na-hivi* ikiwa wewe ni Masihi. Hebu tukuone . . .” Hilo kundi la—la shirika la wahudumu wa Yerusalemu, mnaona, ama, wa Yeriko. “Hebu tukuone ukifanya jambo fulani. Mnaona, niliwaambia; hakuna kitu kwake.”

Yeye hawajali pepo. Bado hawajali, mnaona, kwa hiyo, Yeye—Yeye hufanya jinsi Baba anavyomwonyesha, Yeye alisema.

¹⁶⁴ Lakini maskini ombaomba huyo kipofu huko, akisema, “Loo, Ewe Mwana wa Daudi,” Naye akasimama. Ndugu, ningetaka kuwahubiria wakati mmoja, *Naye Akasimama*. Naam, bwana. Alisimama, na wakati alipofanya hivyo, aligeuka. Sasa, sauti yake, Yeye hakuisikia; hakika hakuisikia. Bali imani yake ilimsimamisha. Imani yake ilimsimamisha nao wakamleta huko.

Yeye akasema, “Ungetaka, nikutendee nini?”

Akasema, “Bwana, kwamba nipate kuona.”

¹⁶⁵ Akasema, “Imani yako imekuokoa.” Mnaona, kama alikuwa na imani ya kutosha kumsimamisha, imani ya kumgusa . . . Hamwoni vile hilo linalingana na Maandiko mengine? Mnaona? Kama alikuwa na imani ya kutosha kumsimamisha, vema, basi alikuwa na imani ya kutosha kukubali uponyaji wake. “Imani yako imekuokoa. Imani yako ilifanya hivyo.” Naye akatembea ameelekeza kichwa chake Yerusalemu, loo, jamani, akielekea Yerusalemu.

¹⁶⁶ Ninaweza kumwona kipofu Bartimayo amesimama pale, akisema, “Yeye aliniambia, Yeye aliniambia imani yangu. Imani ipi? Imani ambapo ninaamini ya kwamba Yeye alikuwa Masihi. Angewezaje kunisikia, nami nimeketi huko nyuma kabisa yadi mia mbili ama mia tatu nimeegemea ukutani? Na hao wote wakipiga makelele na kupiga mayowe, nao watu wakitenda jinsi walivyokuwa wakitenda, inawezekanaje . . .? Mbona, nilikuwa na imani ya kutosha kuamini, nami nikamsimamisha, Naye akaniambia . . . Aisee, na—na—naweza kuiona mikono yangu!”

Nayo Biblia ilisema ndiposa yeye alimfuata, akishangilia na kumsifu Mungu.

¹⁶⁷ Imani ya ombaomba mmoja kipofu ilimsimamisha akiwa kwenye huduma kama hiyo. Imani ya mtu mmoja hapa usiku wa leo inaweza kumleta kutoka Utukufuni moja kwa moja kwenye jengo hili, hakika itamleta. Yeye anaweza kukuponya. Yeye anaweza—Yeye anaweza kukupa ukombozi.

¹⁶⁸ Nilisoma hadithi ndogo juu ya kipofu Bartimayo. Kabla sijafunga, wakati wangu umekwisha; lakini ningetaka tu kusema jambo hili kabla sijafunga, ndipo tutafanya wito wa madhabahuni. Sasa, angalieni tu kwa dakika moja.

¹⁶⁹ Nilisoma hadithi. Labda ilikuwa ni ya kubuniwa. Labda ilikuwa, sijui. Bali nilikuwa nikisoma juu ya kipofu Bartimayo, kasema alikuwa kipofu tangu alipokuwa m—mvulana mdogo, ambapo aliingia upofu. Bali alikuwa ameo, naye alikuwa na mke na maskini msichana mdogo mwenye nywele zilizojiviringa ambaye hakuwa amemwona maishani mwake. Basi ilisema usiku mmoja aliugua. Nao wakamwambia, hiyo hadithi ilisema, ya kwamba yeye alikuwa na hua ambao angeenda nao huko nje. Wangefanya vitimbi kidogo mmoja juu ya mwingine, na hilo lingevutia usikivu wa—wa mpitaji. Nao wangewaangalia maskini hao hua wadogo wakifanya vitimbi wao kwa wao, nao watu wangesimama na kucheka kidogo, kisha wanampa sarafu. Hivyo ndivyo wangali wanafanya.

¹⁷⁰ Na kwa hiyo msichana wake mdogo akashikwa na ugonjwa. Wakamwita daktari, naye daktari akasema, “Vema,” kasema, “kuna homa kali sana juu ya huyu mtoto. Si—sidhani huyu mtoto ataishi, Bartimayo. Hatuna kitu cha kutulizia homa hiyo, kwa hiyo si—sidhani huyu mtoto ataishi.”

¹⁷¹ Ndipo Bartimayo akasema tu. . . Labda aliondoka akaenda kando ya kibanda chake kidogo cha matofali, na kusimama huko nje, naye akasema, “Yehova, kama Wewe utamponya tu msichana wangu mdogo wala usimwache afe, ninakuahidi Wewe, kesho, nitakufanyia dhabihu ya hua wangu wawili wadogo.”

¹⁷² Mnaona, kitu fulani kinachokupasa kusalimisha; watu wanafikiri siku hizi ni kwa sababu tu wanafanya kitu fulani kidogo. La, ni kitu fulani ambacho kweli kinaumiza, kitu fulani kinachokubidi kuchimbua chini kabisa kukipata. Hicho ndicho aina ambayo Mungu huona. “Nitakupa maskini hua wangu wawili na niendelee tu bila wao.” Ndipo ikasema kesho yake asubuhi ninii yake. . .homa ilikuwa imekwisha. Akaenda akawatoa dhabihu wale hua wawili.

¹⁷³ Ikasema wakati fulani baadaye mke wake alishikwa sana na ugonjwa. Na kwa hiyo tabibu akaja na kusema, “Mbona, ninaamini atakufa. Siamini kamwe atapona, Bartimayo,” baada ya kumchunguza kwa muda. Naye akasema, “La, mimi. . .Dawa

yangu haitamsaidia. Yeye atakufa.” Kwa hiyo akatoka nje ya nyumba tena.

¹⁷⁴ Nanyi mnajua hawa mbwa wanaowaongoza watu siku hizi? Nimesahau vile mnavyowaita: mbwa wa jicho lionalo, wanawaongoza. Lakini mbwa siku hizo, wao walisema, walikuwa na wana-kondoo waliowaongoza. Na kwa hiyo Bartimayo alikuwa na mwana-kondoo wa jicho lionalo. Kwa hiyo akasema, “Kama, Bwana, kama Wewe utamponya mke wangu, wala usimwache mwenzangu wa thamani afe, vema, ninakuahidi Wewe, kesho, nitakupa mwana-kondoo wangu.” Ndipo kesho yake mkewe akapata nafuu.

Kwa hiyo alikuwa akipanda kwenda kumtoa huyo mwana-kondoo. Ndipo kasema, kuhani akasema, “Unaenda wapi wewe, Bartimayo kipofu?”

¹⁷⁵ Akasema, “Ninapanda kwenda kwenye—kwenye—dhabihu kumtoa mwana-kondoo wangu kwa Yehova. Nilimwahidi kwamba ningempa mwana-kondoo wangu kwa sababu Yeye alimponya mke wangu.”

¹⁷⁶ Akasema, “Loo, Bartimayo, huwezi kumtoa mwana-kondoo huyo.” Kasema, “Nitakupa pesa kidogo, ndipo uende ukajinunulie mwana-kondoo, ndipo ukamtoe mwana-kondoo huyo. Umnunue huyo kwenye wabadilishaji huko...huko uwanjani.”

Akasema, “Loo, kuhani hilo ni jema kwako. Bali kamwe sikumwahidi Mungu mwana-kondoo *fulani*; nilimwahidi mwana-kondoo *huyu*.” Jambo ndilo hilo.

“Nitamleta mtu mwingine. Nitafanya tendo zuri,” lakini vipi kuhusu wewe mwenyewe. Unaona?

“Nilimwahidi Mungu mwana-kondoo *huyu*.”

¹⁷⁷ “Nilimwahidi Mungu kama angenionyesha tu Uwepo Wake, ningemwamini kwa moyo wangu wote. Sio Binti Jones angemwamini Yeye, bali mimi ningemwamini Yeye kwa moyo wangu wote.” Jambo ndilo hilo. Unaona?

“Nilimwahidi, sio mwana-kondoo *fulani*, bali mwana-kondoo *huyu*.”

Yeye alisema, “Bartimayo, huwezi kumtoa mwana-kondoo huyo. Mwana-kondoo huyo ndiye macho yako.”

Yeye akasema, “Kama nikitimiza ahadi yangu kwa Yehova, Mungu atatoa mwana-kondoo kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu.”

Kwenye asubuhi hii baridi ya majira ya kuchipua Mungu alimtoa Mwana-Kondoo kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu. “Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.”

¹⁷⁸ Mwana-kondoo yuyo huyo ametolewa kwa ajili ya kila mwenye dhambi, kwa kila mgonjwa. Mungu amemtoa Mwana-

kondoo kwa ajili ya macho yetu ya kiroho, na kwa ajili ya macho yetu ya kimwili, kwa ajili ya hali yetu ya kimwili, kwa ajili ya hali yetu ya kiroho. Yeye ni Yehova-yire ambaye tayari amemtoa Mwana-kondoo kwa ajili ya upofu wetu, tupate... tukiuona ulimwengu, tusuone tena ila tumwangelie Yeye; tukiwa wagonjwa, ili kwamba sisi—sisi tuweze kujua ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu kwa ajili ya maombi.

¹⁷⁹ Yupo mwenye dhambi hapa angetaka kusema, “Ndugu Branham, unikumbuke. Na—na—na—nalia sana, ‘Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu. Unirehemu. Ni—ni—ninataka kupata macho yangu ya kiroho. Ninataka kukuona kama ulivyo Wewe, Mwana wa kweli wa Mungu. Unirehemu, Mwana wa Daudi’”? Mwaweza kumwinulia Yeye mikono yenu? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Huko juu kwenye roshani? Inua mkono wako, useme, “Ninataka kumwona, mimi—mimi... Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, Ewe Mwana wa Daudi.” Mungu akubariki, ndugu yangu, huko juu sana katika roshani.

¹⁸⁰ Mtu mwingine, baadhi ya jamaa wadogo walioisikia hadithi yangu ndogo kuhusu maskini Bartimayo hapo alipokuwa mdogo? Unajua, mama yako, labda, alikuweka wakfu kwa Mungu, pia, wakati ulipozaliwa. Mnaona, hatimaye Bartimayo alitimiza lile agizo ambalo Mungu alikuwa amemwekea hapo mama yake alipomweka wakfu. Labda usiku wa leo huenda macho yenu madogo yatafunguka, enyi jamaa wadogo, nanyi mtamwona Mwana-Kondoo wa Mungu. “Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.”

¹⁸¹ Waweza kuinua mkono wako, mtu mwingine? “Unirehemu, Ewe Mwana wa Daudi.” Mungu ambariki msichana huyu mdogo. Mungu ambariki msichana huyu. Mungu ambariki mama huyu anayeketi hapa. Mungu ambariki mvulana huyu mdogo hapa. “Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.” Huyu mwanamume hapa, naam, Mungu akubariki. Mtu mwingine mkono wangu wa kulia? “Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.”

¹⁸² Imani yako inaweza kumgusa Yeye, imshushe hapa chini moja kwa moja kama vile ya Bartimayo ilivyofanya. Yeye hayuko katika yoyote... Yeye atasimama na kuondoka Mbinguni kuja kwenye kanisa la Assembly of God usiku wa leo kuonyesha rehema, iwapo utakuwa tu na imani ile ile ambayo Bartimayo alikuwa nayo. “Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.” Kungekuwako na mwingine mahali fulani jengoni ambaye hajainua mkono wao? Kumekuwako na kama kumi ama kumi na wawili walioinua mikono yao kwamba walitaka kupata rehema; “Ewe Mwana wa Daudi.”

¹⁸³ Niliona jana usiku... Kuna msichana mdogo aliyeketi hapa, anaonekana yuna umri wa yapata miaka kumi. Aliinua mkono

wake dakika chache zilizopita. Alimtaka Yesu. Yapata umri wa maskini mtoto wangu Becky, nadhani, huko nyumbani mtoto wangu Rebekah. Nami nilimwona maskini msichana mdogo akija huku juu jana usiku, wakati aliposimama madhabahuni. Mara tu aliposimama pale, alianza kunena kwa lugha. Mtu fulani aliniambia, baadhi ya ndugu, ya kwamba alikuwa akikimbia kote kanisani, akinena kwa lugha na kuimba kwa lugha na kila kitu. Jinsi ambavyo Bwana alimbariki msichana huyo mdogo. Akampata wakati moyo wake ni mdogo na mwororo, kabla hajapitishwa kwenye maskini magazeti ya *Hadithi ya Kweli* na uchafu wa ulimwengu, yakaukausha moyo wake kabisa. Ninapenda kuona watoto wadogo wakija.

¹⁸⁴ Mungu: uyaweke maisha yako wakfu Kwake. Yeye atakutendea jambo fulani pia, kipenzi. Hakika atakutendea. Mtu mwingine sasa kabla hatujaomba? “Bwana, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.”

¹⁸⁵ Baba yetu wa Mbinguni, ninawakabidhi Kwako. Waliinua mikono yao. Wao ni watoto Wako kwa imani katika Yesu Kristo. Wanajua ya kwamba Wewe upo hapa, Baba. Wanajua ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu. Wanaamini sasa ya kwamba kwa kuwa Wewe ulisema nao mioyoni mwao ya kwamba wako tayari kukupokea Wewe kama Mwokozi wao, kwa sababu ilikubidi kuzungumza kwanza. “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu,” alisema Bwana Yesu, “asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba, watakuja.” Na sasa, Bwana, wao wanakuja usiku wa leo juu ya msingi wa Damu iliyomwagika ya Bwana Yesu. Ndipo kama kasisi wao, ama mchungaji wao—wao, ama mtumishi, na—naomba, Baba, maombi yangu ya imani yanaenda Kwako.

¹⁸⁶ Na kuwaacha wajue ya kwamba wameokoka, ninakunukulia Wewe Neno Lako. Wewe ulisema, “Yeye alisikiaye Neno Langu...” Nimeendelea kulinukuu kwa saa moja iliyopita ama zaidi. “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna, wakati uliopo, Uzima wa Milele wala kamwe, kamwe hataingia hukumuni; bali tayari amepita kutoka hukumuni kuingia Uzimani.” Baba, hivyo ndivyo Wewe ulivyosema. Waliinua mikono yao ya kwamba waliliamini. Nao wa—waliliamini; wamelipokea. Kwa hiyo sasa ninajua ya kwamba Wewe umewapa Uzima wa Milele, na Wewe utawafufua tena katika siku za mwisho. Ulisema ya kwamba Wewe ungelifanya. Uliahidi ya kwamba Wewe ungelifanya, na Wewe ni Mungu na hutimiza ahadi Zako zote. Ahadi Zako ni ndiyo na amina, kwa hiyo huwezi kughairi ahadi Yako. Wewe—Wewe ulisema ungelifanya na ukaahidi kulifanya.

¹⁸⁷ Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utawapa ujasiri kuwafanya wajue ya kwamba Roho huyo aliyekuwa karibu nao, akisema, “Mtoto, umekosea. Unapaswa kunipokea usiku wa leo. Nitasimamisha ratiba Yangu yenye shughuli nyingi na kugeuka

na kusema, ‘Dhambi zako zimesamehewa. Nenda na usitende dhambi tena.’” Kama vile umesema mara nyingi sana, Wewe utawaambia usiku wa leo, kwa sababu wamefanya uamuzi wao.

¹⁸⁸ Sasa, Baba Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe hutamwacha mmoja wao...Siamini ya kwamba waliinua mikono yao kwa kusema tu kuinua mikono yao. Ninaamini walikuwa ni waaminifu; kweli walilimaanisha. Na sasa ninawakabidhi Kwako, na kuomba ya kwamba Wewe uzisamehe dhambi zao zote. Ninawaomba kwa moyo wangu wote, ya kwamba Wewe utawasamehe dhambi zao, kila mwenye dhambi humu ndani, kwamba Wewe utasamehe dhambi zao zote.

¹⁸⁹ Baba, kundi hili dogo, ninataka kukutana nao kule kwenye ile siku kuu ya Unyakuo tutakapokusanyika, niwaone wakija kutoka taifa hadi taifa, wakikusanyika. “Sisi tulio hai na tuliosalia hatutawatangulia wale waliokwisha kulala mauti.” Parapanda italia, na waliokufa watafufuka kwanza, ndipo tutakutana nao, kisha tunyakuliwe pamoja nao kumlaki Bwana hewani, na hivyo tuwe pamoja na Yeye milele. Bwana, ninajua ya kwamba Wewe ulisema hivyo katika—katika Kitabu cha Wathesalonike, mlango wa 5, nami ninajua kwamba ni kweli. Nami nitakutana nao kabla hatujakutana Nawe. Kwa hiyo tuna furaha sana kwa ajili ya hili.

¹⁹⁰ Nasi tunaamini sasa ya kwamba...Ninaamini kwa moyo wangu wote, ya kwamba kwa sababu waliinua mikono yao, na kwa sababu kwamba nimeomba na kuuliza na kufuata mwongozo wa Roho vizuri nijuavyo mimi, ya kwamba wamesamehewa dhambi zao. Sasa, wana furaha kwa ajili yake, Bwana. Sasa, kuna jambo moja zaidi ulilowaagiza kufanya. “Yeye atakayenikiri Mimi mbele ya wanadamu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu.”

¹⁹¹ Huu utakuwa ni usiku ambao kamwe hawatausahau, vijana hawa, kukumbuka kwamba mtoto Bartimayo aliisikiliza hadithi ya mama yake, na kujua ya kwamba siku moja Mungu alimtumia. Na hii ndiyo saa ambayo Wewe unawatumia, unawatumia na kuwaingiza katika Ufalme Wako. Walio na umri mkubwa zaidi walioinua mikono yao, hao walikuwa ndio, labda kama Bartimayo baadaye, aliyekuwa kipofu lakini akafunguliwa macho, macho yake ya kiroho. Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utawafanya wawe watoto Wako usiku wa leo, nao watajiunga na kanisa zuri, na—na kubatizwa kwa ubatizo wa Kikristo, na kumpokea Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana.

¹⁹² Sasa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, nitaona na kuwauliza, ninyi ambao mlikuwa waaminifu sana, kama mnaniamini kuwa nabii wa Mungu, ama, mtumishi Wake, hasa, kama mnaniamini mimi kuwa mtumishi Wake kwa moyo wenu wote, nanyi mnaamini ya kwamba nimewanukulia ile

kweli, mlilisikia Neno: “Yeye alisikiaye Neno Langu . . .” Yohana Mtakatifu 5:24. “. . .na kumwamini Yeye aliyenipeleka . . .” Nimelithubiri Neno; ulimwamini Mungu, nawe ukainua mkono wako ya kwamba ulikuwa mwenye dhambi, wala hukutaka kuwa mwenye dhambi tena. Basi Mungu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu.” Basi ni kitu gani kilichouvuta mkono wako juu? Mungu. Ulifanya uamuzi wako. Vema, sasa, Yeye alisema nini? “Yeye anijiaye Mimi sitamtupa nje kamwe.”

¹⁹³ Basi wewe ni Mkristo, iwapo kweli ulimaanisha hilo. Nyinyi wavulana na wasichana wadogo, nanyi wenye umri mkubwa zaidi, katika umri wenu wa makamu, na utineja wenu, ninyi nyote, ninyi ni Wakristo mnapoliamini.

¹⁹⁴ Sasa, kunalo jambo moja bado hamna budi kufanya. Kama kweli unaamini hilo kwa moyo wako wote, nitakuomba usimame tu kwa miguu yako, na kusema hivi kwa kusimama, haikubidi kusema neno moja, lakini simama tu upate kushuhudia kwa watu ya kwamba, “Sasa nakiri dhambi zangu zote, na kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu.” Sasa, ninyi ambao mmemkubali hivyo, simameni kwa miguu yenu.

¹⁹⁵ Vipi kuhusu jambo hilo, msichana mdogo, uliyekuwa umeketi hapa? Unaamini Yeye ni Mwokozi wako? Hiyo ni kweli. Simama papo hapo, kipenzi. Mvulana mdogo huku, yeye ni . . . Vema. Nyinyi huko nyuma, ninyi huko juu kwenye roshani, mvulana mdogo na msichana huko kwenye roshani, sawa. Popote jengoni sasa ambaye umemkubali Yesu kama Mwokozi wako, simama. “Yeye atakayenishuhudia mbele za watu, yeye anishuhudiaye mbele za watu, huyo nitamshuhudia mbele za Baba Yangu na watakatifu . . .”

¹⁹⁶ Sasa, kunao baadhi yenu watu wenye umri mkubwa mlioinua mkono wenu. Hawa hapa mmoja, wawili, watatu, wanne, ninawaangalia watoto wanne wamesimama juu ya hadithi yangu ndogo usiku wa leo ya Bartimayo. Sasa, vipi kuhusu baadhi yenu nyinyi mlio na umri mkubwa ambao mliinua mkono wenu? Hivi nyinyi. . .? Mnaona jinsi maskini mioyo yao ilivyo myororo? Wa—wanaamini na kwa hiyo wananinii tu, wanasimama, wanasimama ili kumkubali Yeye. Hivi mnaamini wamesamehewa? Hakika wamesamehewa. Hakika wamesamehewa.

¹⁹⁷ Sasa, baadhi ya wengine wenu wanaotaka kumkubali na kusema, “Nitashuhudia hadharani.” Biblia ilisema wote walioamini waliongezwa kwa kanisa. Mnaamini ya kwamba Yesu anasamehe dhambi zenu usiku wa leo? Simameni kwa miguu yenu pamoja na watoto hawa. Ni wangapi watakaofanya hivyo sasa hivi? Vema, Mungu awabariki. Mvulana huyo aliye kwenye kiti cha magurudumu, mvulana huyu hapa, msichana

huyu hapa, mama huyu, hilo ni zuri; sawa. Mtu mwingine aseme, “Ninamkubali Yeye sasa hivi juu ya . . .”

¹⁹⁸ Sasa, usininii. . . Hakuna hisia. “Sitafuti hisia. Ninatafuta kwa sababu Yeye aliniahidi, ‘Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.’” Juu ya misingi hiyo katika dhambi zako zilizoungamwa, na kutambua ya kwamba wewe ni mwenye dhambi, basi utasimama na kumkubali Yeye kama Mwokozi wako, simama.

¹⁹⁹ Mmoja, wawili, watatu, wanne, watano, sita, hivi hakuna mwingine mmoja? Mmoja zaidi ambaye ningeweza kukuombea kabla hamjaketi chini? Kuna mmoja zaidi? Yeyote miongoni mweni huko nje u—ukumbini atakayesimama? Mungu akubariki, mama. Hilo ni zuri sana. Vema, kuna mwingine? Mungu akubariki, dada. Vema, kuna mwingine? Wapo saba. Hiyo ni namba kamilifu. Sasa, hebu tuinamishe kichwa chetu. Endeeleni tu kusimama.

²⁰⁰ Baba yetu wa Mbinguni, ni . . . Neno Lako haliwezi kushindwa; ni la Milele. Wewe ulisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele. . .” Ulisema hivyo, Bwana. “. . . wala hataingia hukumuni, ama, kuhukumiwa hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani,” kwa sababu wamemwamini Bwana Yesu Kristo, kwamba Yeye alikufa badala yao, akizichukua dhambi zao. Na kupitia kwa maovu yao wanafanywa haki ya Mungu kupitia kwa Yesu Kristo. Hao hapo, Baba. Wao ni kumbukumbu za ujumbe. Wako hapa. Wao ni watoto Wako.

²⁰¹ Sasa, huenda kamwe nisiweze kuwapa mkono katika dunia hii. Lakini, Baba Mungu, juu ya msingi wa Neno Lako ninaamini na kulikubali Neno Lako ya kwamba Wewe ni Mungu, wala huwezi kusema uongo, nalo Neno Lako ni la Milele. Ninawadai kwa ajili ya Injili. Ninawadai, kwa ajili ya Mungu, kupitia Yesu Kristo, akiwaondolea dhambi zao zote.

²⁰² Pia, Baba, ninaomba ya kwamba utawaongoza watoto hawa waingie katika Uzima wa Milele. Waongoze kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu. Wabatize, Baba, katika Roho na nguvu za Mwili wa Yesu Kristo, kusudi wapate, kuona kwa macho yao wenyewe, ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu. Wameliamini kwa imani sasa na kulikubali, na juu ya misingi hiyo ulisema waliokolewa. Ninawaombea na kuwakabidhi mikononi Mwako, katika Jina la Yesu Kristo.

²⁰³ Sasa, unapowaona watu wakisimama, inua kichwa chako, wale wanaosimama, ninawatakeni muwape mikono wanapoketi chini. Huko juu kwenye roshani, kule, papa hapa, mwajua, enyi Wakristo mlio karibu nao sasa, ninyi, mnapoketi, wapeni tu mkono, msemi, “Mungu akubariki.” Mpe mkono mvulana huyu

mdogo hapa. Mungu aubariki maskini moyo wake hapo. Baadhi yenu akina mama mnaoketi hapo, papa hapa. Hiyo ni kweli. Mungu awabariki.

²⁰⁴ Mungu akubariki, ndugu, mwenye mguu uliovunjika hapo. Usijali, utakuwa sawa. Nilijua hilo siku chache zilizopita usiku, kwa hiyo kamwe usijali hilo. Uko sawa. Kwa hiyo, huko juu kwenye roshani, wote, ninaona, ni—ni wote, vema. Loo, si Yeye ni wa ajabu? “Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.”

²⁰⁵ Aisee, “Ndugu Branham, unaamini hiyo kuwa ni kweli?” Mbona, hakika ninaamini hiyo kuwa ni kweli. Nisingesimama hapa na kuhubiri kitu fulani nisichokiamini. Ninapata matatizo wakati wote kwa kuhubiri mambo ninayoamini. Hivyo ndivyo linavyoishia. Mimi... Lakini ninaliamini kwa kuwa Mungu alisema hivyo, na hilo latosha kwangu mimi. Ninaamini ni kama tu... kwamba watu hao, msichana huyo mdogo, wavulana wadogo, na hawa watu hapa walimwita kutoka Utukufuni kama vile tu Bartimayo kipofu alivyomsimamisha akienda Zake. Mnaamini hilo?

²⁰⁶ Ni wangapi wenu walio wagonjwa? Inueni mikono yenu, walio wagonjwa na wahitaji. Amina. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Mungu yule yule... Sijui. Vema. Mimi—mimi... Kitu fulani kilinigusa basi. Yeye yupo hapa. Malaika wa Bwana mnayemwona kwenye ile picha, Mungu akiwa ni Hakimu wangu, kwenye Siku ya Hukumu mtajua Yeye yupo papa hapa sasa. Hiyo ni kweli. Malaika wa Bwana yupo hapa.

²⁰⁷ Mtu fulani mahali fulani, mahali fulani anateseka. Wao wananinii... wana imani. Kitu fulani kimejongea. Mtu fulani amefanya jambo fulani mahali fulani, ama ametenda jambo fulani. Yeye asingekuja namna hiyo, nami nikijaribu kuishikilia hii kuwa ni ibada ya Injili.

²⁰⁸ Mna kadi zozote za maombi? Hamna? Vema, hamzihitaji. Hamzihitaji. Iweni na imani na muamini. Kama nimewaambia... Nyinyi waongofu wachanga hapa, kwa kuwa Yeye yupo hapa... Ee, marafiki, kamwe hamtajua ni hisia ya jinsi gani iliyopo wakati Yeye—wakati Yeye anapokugusa. Unajua yale unayozungumzia basi. Hiyo ni kweli. Naam, unajua yale unayonena habari zake. Loo, nina hakika tu kadiri niwezavyo kuwa. Iweni na imani sasa. Aminini tu.

²⁰⁹ Sara aliketi hemani naye akasema moyoni mwake, akacheka, naye yule Malaika akageuka na kusema, “Kwa nini Sara akacheka, akisema moyoni mwake ya kwamba hili lisingewezekana?” Hiyo ni kweli? Vipi kuhusu mwanamke aliyeligusa vazi Lake Naye akaangalia? Hivi hamuamini ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule usiku wa leo?

²¹⁰ Sasa, ninyi waongofu wachanga, ninataka kuwathibitishieni ya kwamba Yule mliyemgusa, dada kipenzi hapa, wewe na kijana... dada anayeketi hapa, na huyo ndugu, huyo mvulana

mdogo, na mvulana huyo mdogo na msichana anayeketi hapo, ninataka kuwaonyesha ya kwamba ilikuwa ni Bwana Yesu yeye yule aliyefanya ile ahadi.

Loo, jamani. Loo, laiti ningalijisikia hivi wakati wote. Kweli. Mwaminini Mungu. Ombeni, ninyi nyote. Iweni tu katika maombi.

²¹¹ Nitawapa kisogo. Yule Malaika wa Bwana alifanya nini? Kuwaonyesha tuko katika siku za Sodoma, kuwaonyesha tuko katika siku ya mwisho, ya kwamba nchi hii hapa ni Sodoma mamboleo, kuwaonyesha ya kwamba yule Malaika wa Bwana angali ni Malaika wa Bwana. Sasa, hamna kadi za maombi, kwa hiyo hatutakuwa na mstari wa maombi. Lakini haiwabidi kuwa na kadi za maombi. Jambo pekee ninalowaomba kufanya ni kuamini ya kwamba nimewaambia kweli, kweli ya Injili, na ni Mungu.

²¹² Nitawaangalia wahudumu hawa hapa nyuma. Mnaamini hili, ndugu? kwa moyo wenu wote? Mnaamini ile Injili nimekuwa nikihubiri ni ya kweli? Mungu aibariki miyo yenu. Kuna hisia nzuri sana nyuma yangu, imani yenu ndugu. Wakati mwingi juma hili imetokea kwamba nimechanjachanja na kukatakata na kila kitu kingine. Sitaki mfikirie nimewaudhi. Ninawapenda. Ninyi ni ndugu zangu. Lakini ninyi wenyewe mnajua ya kwamba kanisa linaondoka. Hatuna budi kulirudisha, kulirudisha. Hatuna budi kulirudisha.

²¹³ Sasa, hii hapa. Yupo mwanamke mbele yangu. Ninamwangalia moja kwa moja. Mtu fulani huko nje anamgusa Kuhani Mkuu. Ninaiona sura yake *hapa*. Hebu kidogo, mtu fulani alimgusa Yeye, sawasawa na vile mwanamke alivyomgusa Bwana wetu Yesu. Hivyo ndivyo mwanamke huyu amefanya, nami ninatenda tu mahali Pake. Mnaona? Hivi nyote... Mnaelewa? Sasa, itakuwa... Nitalishika kwa dakika moja tu. Mnaona, wakati likija kutoka... Sasa, mtu fulani na amguse. Kila mmoja wenu anaomba. Amini sasa kwa moyo wako wote. Ketini kimya kabisa; aminini.

²¹⁴ Naam, bwana. Ni mama anayeketi moja kwa moja hapo pembeni. Naam, hiyo ni kweli. Unayo kadi ya maombi? La wewe... Ninajua huna kadi ya maombi. Sikujui mimi; Mungu anakujua. Unaona, hivi nyote...? Ninawatakeni ninyi nyote mwangalie upande huu. Hivi hamwezi kuiona ile Nuru imening'inia juu ya yule mwanamke pale? Mnaiona ile—ile ndogo... papo hapo juu yake. Mnaiona ile Nuru inayoonekana ya kiajabu imening'inia juu yake pale? Sasa, angalieni, inafunguka. Huyo mwanamke amechunguzwa na daktari wa namna fulani, nao wakamwambia alikuwa na uvimbe, namna fulani ya... Anangojea upasuaji, bali hatapokea huo upasuaji. Anajaribu kumtumainia Bwana kwa ajili ya uponyaji wake. Hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama.

215 Sasa, enyi waongofu wachanga, yule mama anayeketi papo hapo karibu naye hapo, alionekana kuwa ni...Nuru ile ilijongea moja kwa moja juu ya mama huyo anayeketi papo hapo karibu naye. Hiyo hapo tena. Nilidhani ilirudi kwa huyo mama, bali ilimwendea mama *yule*. Yeye ni mwaminio, Mkristo mwaminio. Yeye ana namna fulani ya ninii, kitu kama mzio, ama, unatokea mikononi mwake. Hiyo ni kweli. Sikujui mimi, sivyo, mama? Huna kadi yoyote ya maombi, hakika. Unaamini ya kwamba utapona? Unaamini huyo alikuwa ni Mungu? U—unaamini ya kwamba—ya kwamba...ya kwamba ninaweza kukwambia yale unayoombea? Unaamini hilo? kwa Mungu. (Nyamazeni, nyamazeni, ketini, mnaona, tafadhalini.) Unaamini? Bibi Bossler, unaamini sasa ya kwamba utaponywa? Mungu akubariki. Hivyo ndivyo unavyoitwa, sivyo?

216 Vipi kukuhusu wewe, jamaa mdogo, unayeketi papa hapa? Ndiyo Hii papa hapa kwako. Unaamini? Ninaona kidogo mabega yako yameinama, namna *hiyo*. Lakini kuna kitu kingine mbali na hicho kinachokutatiza. Kama Mungu ataniambia shida yako, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, mtumishi Wake? Unaugua ugonjwa wa tumbo. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Um-hum. Si kidonda, wewe una wasiwasi tu na kuchafuka kwa tumbo lako, ndiko kunakosababisha hilo. Hiyo ni kweli kabisa. Iwapo unaamini kwa moyo wako wote...

217 Unaamini? Sasa, iweni na kicho kabisa. Msisogee. Mnaona, wakati wowote unaposogea hilo—hilo—hilo linasababisha jambo fulani. Mnaona? Iweni na kicho. Vipi kuhusu mtu fulani upande *huu*? Imekuja *huku*, sasa hebu twende *huku*. Mnaamini? (Tutakapowapata watatu ama wanne, aseme—aseme jambo fulani.)

218 Iweni na imani; msitie shaka. Inanibidi tu kuangalia popote la—laiti ningaliweza kusema tu *huyu* ama *yule*. Siwezi. Inanibidi tu kuangalia. Imani haifahamiki kabisa na watu.

219 Maskini mama anayeketi papo hapo akiniangalia. La, ninii...papo hapo nyuma yako, dada, papo hapo...Naam. Una shida na macho yako, hiyo ni kweli. U—unaamini Yeye atakuponya hayo? Iwapo huamini, utayapoteza macho yako; yanaendelea kuzima zaidi na zaidi wakati wote. Wewe amini tu kwa moyo wako wote. Unaamini Mungu anaweza kuniambia kwamba wewe ni nani? Unajua mimi sikujui. Bi. Johnson, unaweza kwenda nyumbani ukapate afya, mwamini Bwana.

220 Mama anayeketi papo hapo karibu naye, ilikubidi kuamka na kuondoka dakika chache zilizopita. Shetani alijaribu awezavyo kukunyang'anya huu. Unaamini Mungu anaweza kuniambia kuhusu shida yako? Ungeweza kunikubali mimi kama nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Unaamini hilo kwa moyo wako wote? Sikujui mimi. Sijawahi kukuona maishani mwangu, bali wewe kweli umewasiliana na Mungu sasa hivi.

Kweli. Wewe ni mgonjwa sana. Hiyo ni kweli. Ni ugonjwa wa kibofu nyongo. Hiyo ni kweli. Jambo lingine, una moyo uliotanuka. Hiyo ni kweli kabisa. Bi. Miller, inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Nenda, ukaupokee uponyaji wako. Yesu Kristo anakuponya.

²²¹ Ninakupa changamoto kuamini hilo. Ni—ninaninii tu—ninakuomba tu uamini. Vema, mwamini Mungu. Unamwamini? “Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu.” Unamwamini Yeye kwa moyo wako wote? Basi nisikieni, sikilizeni. Ni waaminio wangapi walio hapa? Inua mkono wako. Vema, ikiwa wewe ni mwaminio, sasa, weka mkono wako chini. Kila mmoja wenu ni waaminio. Ni wangapi walio wagonjwa? Inueni mikono yenu. Vema, waaminio wekeaneni mikono. Nitalinukuu Neno lile lile. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Jambo ndilo hili. Mnaliamini? Sasa, wewe mwombee mtu fulani. Wewe mwekee mikono mtu fulani karibu nawe, kando yako, huko juu kwenye roshani. Naam, aminini.

²²² Huyu mama aliyeketi huko nje pale katikati, anayeugua ugonjwa huo wa wasiwasi, uliosababishwa na... Vema, jambo ndilo hilo dada, sikujui mimi, sijawahi kukuona maishani mwangu. Hiyo ni kweli? Lakini umekuwa na wasiwasi, loo, kwa miaka kadhaa. Kristo anakuponya, anakupa afya.

Huko juu kabisa kwenye roshani. Amina. Yeye anamponya kila mmoja wenu kama mtaamini. Sasa, ombeaneni. Wekeaneni mikono.

²²³ Baba wa Mbinguni, imani ya watu hawa ilimrudisha Bwana Yesu Kristo katika umbo la Roho Mtakatifu miongoni mwao usiku wa leo, akiwaokoa waliopotea na kuwaponya wagonjwa. Ee Bwana, wao ni waaminio. Wamewekeana mikono. Wanaamini ya kwamba ni wewe yule jana, leo, na hata milele, na Mungu yule yule. “Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi,” wanasema kwa sauti kuu. Jalia nguvu zilizomfufua Yesu kutoka kaburini ziwainue kwa miguu yao wakiwa na ushuhuda, wakipiga makelele na kuusifu utukufu wa Mungu. Jalia wasimame kama Bartimayo, wakiiangalia mikono yao mpaka waone ya kwamba nguvu za Mungu zimewaponya. Lijalie, Bwana.

Sasa, endeleeni kuomba, endeleeni kuomba, endeleeni tu kuomba.

²²⁴ Ee Bwana, lipo jambo moja tu lingaliweza kuzuia ibada ya uponyaji mfululizo, na hilo lingekuwa ni kutokuamini. Nimeona kwenye umati ninapoangalia kupitia hapa, Bwana, nikaona huo mchirizi mdogo wa giza ukijaribu kuizuia ile Nuru tukufu ambayo inazungukazunguka huku, ikijaribu kupata njia ya kushuka kupitia giza lile ipate kumgusa mtu fulani.

²²⁵ Ee Baba Mungu, nipe nguvu, nipe imani. Jalia hawa watu waelewe ya kwamba Wewe umethibitisha, Bwana, ya kwamba ninawaambia ukweli. Wewe ulisema ulipokuwa hapa duniani,

“Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini”; na kama sizifanyi kazi za Mwokozi wangu, basi jalia wasiniamini. Lakini Bwana, Wewe unafanya kazi zile zile ambazo ulizifanya wakati ulipokuwa hapa duniani.

²²⁶ Ee Baba, ninaomba sasa ya kwamba wao wataamini kwa sehemu. Nipe imani ya kulivunja hilo giza kutoka juu yao, Bwana, kusudi nguvu hizo na Nuru ya Mungu ipate kushuka juu ya kila mtu hapa ndani, ili iweze kumponya kila mmoja wao.

²²⁷ Shetani, umefichuliwa. Mbona, wewe ni ibilisi, nawe unajaribu kulishika kundi hili la watu. Nakusai katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani ya watu hawa na uachane nao. 

61-0215 Ewe Mwana Wa Daudi, Unirehemu
First Assembly Of God Of Long Beach
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org